# Nipashe

Jumatano Julai 20, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581012 *

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,016,428,582/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#




**Mume** na mke kortini mashtaka kukutwa na meno 413 ya tembo

UKURASA 3



INTER MIAMI KUMSAJILI LIONEL MESSI

UKURASA 21



# Msuya atoa kauli hoja ya Katiba Mpya

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**MWANAFUNZI AUAWA KINYAMA, MWILI WAKE WATUPWA**

MWANAFUNZI wa kidato cha tatu (jina na shule vinahifadhiwa), amekutwa...

UKURASA WA 3

**KORTINI MADAI YA MAUAJI YA MJUKUU**

MKAZI wa Kidodi wilayani Kilosa, Shaibu Mkweche, amefikishwa...

UKURASA WA 4

**PM AAGIZA UFUATILIAJI MAFUNZO UGHAIBUNI**



WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa ameitaka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuendelea kusimamia...

## Utata vifo vya watoto watano wa familia moja

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan akipokea ujumbe maalum kutoka kwa Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Felix Antonio Tshisekedi, uliowasilishwa na Mjumbe Maalum, Prof. Serge Tshabangu, Ikulu Chamwino mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## Hivi ndivyo zitakavyotumika trilioni 2/- za mkopo wa IMF

UKURASA 2


MICHEZO CHICO, YACOUBA WATEMWA YANGA UK.24 MAONI, KATUNI UK.6



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na wanafunzi, walimu na wazee, baada ya kuzindua madarasa mapya saba ya Skuli ya Msingi Mkwajuni, iliyojengwa na Kikosi cha Chuo cha Mafunzo kupitia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya ufadhili wa mkopo wa UVIKO-19, wilayani Kaskazini "A", Unguja jana, akiwa katika ziara ya kutembelea miradi mbalimbali ya maendeleo. **PICHA: IKULU**

# Msuya atoa kauli Katiba Mpya

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI Mkuu mstaafu Cleopa Msuya amesema ni vizuri na muhimu sasa mjadala wa katiba mpya ukafikia mwisho ili watu waendelee na majukumu mengine huku akisisitiza lisiwe la kuzungumziwa kila mwaka.

Msuya aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam baada ya kutoa maoni yake katika kikosi kazi kilichoundwa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya kukusanya maoni na mapendekezo yatakayomwezesha kutimiza majukumu yake ipasavyo.

"Ni vizuri tukafika mwisho na mjadala wa katiba. Tujumuishe mazungumzo yote yaliyofanyika na habari zote zilizokusanywa kama kuna la kuongeza waongeza tupate hiyo katiba. Baada ya hapo watu tufanye kazi, tusiwe kila mwaka watu tunakaa tunarudia katiba," alisema Msuya.

Aliongeza kwa kushauri kuwa asilimia kubwa ya wananchi nchini ni vijana, hivyo kikosi kazi kifikirie suala la kutoa elimu ya uraia mwema kwa vijana kwa mifumo mbalimbali ili kuwajenga Watanzania wa rika la kesho watakaofanana na wazee wazalendo waliopo sasa.

Pia alisema wanataka kuona ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya watu waliotuhumiwa kula rushwa, badala ya kuishia kuhubiri juu ya suala hilo tu.

"Tusihubiri tu rushwa, rushwa. Sasa tufike hatua tusikie na tuone vitendo vya kupambana na wale waliotuhumiwa rushwa," alisema Msuya Msuya ambaye aliwahi kuwa Waziri Mkuu wa Tanzania.

Msuya (91) aliwahi kuwa Waziri Mkuu mwaka 1980 hadi 1983 na baadaye Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais mwaka 1994 hadi 1995.

Nyadhifa zingine alizowahi kushika ni Katibu Mkuu katika wizara mbalimbali na Waziri katika wizara za Fedha (1970 -1975 na 1983 hadi 1989), Viwanda (1975 - 1980) na Viwanda na Biashara mwaka 1990 hadi 1994.

**MACHIFU WANENA**

Naye Chifu wa Simiyu, Tonisiza Sangalali, ambaye aliwakilisha ujumbe wa Mwenyekiti wa Umoja wa Machifu Tanzania, Frank Maleale, katika kikosi kazi hicho, alisema miongoni mwa mambo waliyoyawasilisha ni kusisitiza uchaguzi wa amani na kuwa na utaratibu wa watu kusikilizana.

Pia alitoa wito kwa Watanzania kuona umuhimu wa serikali iliyoko madarakani huku akisisitiza kuwa katika jambo lolote la kitaifa ikiwamo Katiba, watu waende hatua kwa hatua, kwa amani na kwa kusikilizana kwa kuwa ni suala la umuhimu.

"Katiba ni kitu muhimu na nafikiri Rais yuko katika hatua nzuri na analishughulikia kwa uelewa zaidi. Tunahamasisha watu tuendane na serikali ya mama (Samia Suluhu Hassan) na maelekezo tunayofuata kutokana na serikali kuu. Tutakwenda na yale yanayopangwa na serikali inayotuongoza," alisema.

Pia alitoa wito kuendelea kuwapo kwa maelewano na ushirikiano baina ya vyama vya siasa, huku akisisitiza nidhamu ya kumsikiliza Rais.

## Mwanafunzi auawa kinyama, mwili watupwa

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MWANAFUNZI wa kidato cha tatu (jina na shule vinahifadhiwa), amekutwa amefariki dunia baada ya kubakwa, kulawitiwa kisha kunyongwa na mwili wake kutupwa karibu na nyumbani kwao.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Kamishna Msaidizi (ACP) Nicodemus Katembo, alisema jana kuwa tukio lililotokea Jumapili iliyopita mjini hapo.

Alisema baada ya kufanyiwa unyama huo na kufa, mwili wa mwanafunzi huyo ulikutwa umetupwa karibu na nyumbani kwao, Mtaa wa Msufini.

Katembo alisema mwili huo baada ya kufanyiwa vipimo na madaktari, ilibainika kuwa mwanafunzi huyo amelawitiwa, amebakwa kisha kunyongwa na mwili huo kutupwa kwenye maeneo ya nyumbani kwao.

Alisema mwanafunzi huyo anadaiwa kufanyiwa unyama huo na watu ambao hawajafahamika.

Kaimu Kamanda huyo alisema hadi sasa bado chanzo cha mauaji hayo hakijafahamika na upelelezi unaendelea.

Alisema kwa sasa Jeshi la Polisi linaendesha msako mkali ili kuwabaini wahusika wa tukio hilo na hatimaye kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji Masasi, Dk. Emmanuel Sabasi, alisema ni juzi majira ya saa 2:00 asubuhi walipokea mwili wa mwanafunzi huyo na kisha kuufanyia vipimo.

Dk. Sabasi alisema baada ya mwili huo kufanyiwa vipimo vyote, ulibainika kuwa mwanafunzi huyo alibakwa, kulawitiwa kisha kunyongwa.

Alisema ripoti ya vipimo vya mwili wa mwanafunzi huyo tayari wameshaikabidhi katika Jeshi la Polisi kwa ajili ya taratibu zingine husika ziendelee.

# Trilioni za IMF kuleta ahueni mfumuko wa bei

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Fedha na Mipango, imesema kuwa Shirika la Kimataifa la Fedha (IMF), limeridhishwa na utendaji kazi wa Rais Samia Suluhu Hassan, ndiyo maana limeidhinisha mkopo wa masharti nafuu wa Dola za Marekani bil. 1.04 (sawa na Sh. trilioni 2.4) kwa miezi 40, kutekeleza miradi ya maendeleo.

Aidha, fedha hizo zinakwenda kuleta nafuu kwenye mfumuko wa bei kwa kushusha bei ya mafuta na uchumi jumuishi.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Msemaji wa Wizara ya Fedha na Mipango, Ben Mwaipaja, alisema fedha hizo zitatekeleza miradi ya kimkakati ambayo Rais ameipa kipaumbele kwa manufaa ya wananchi.

Gazeti hili lilitaka kujua tafsiri ya mkopo huo kwa nchi, na kuelezwa kuwa zimepatikana baada ya majadiliano ya kina na Bodi ya IMF ambayo sasa imeidhinisha na kinachofuata ni kusaini mkataba wa makubaliano.

"Tunashukuru IMF kwa kuidhinisha fedha ambazo zitaelekezwa kwenye kusisimua uchumi, huduma za kijamii, kuendeleza sekta binafsi. Tulikuwa na mjadala mkubwa sana na IMF hadi kufikia ukingoni sasa tutakwenda kupata Sh. trilioni 2.4 kwa maendeleo ya Watanzania," alisema Mwaipaja.

Msemaji wa Serikali na Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Habari (MAELEZO), Gerson Msigwa, alisema fedha hizo zitaleta nafuu ya mfumo wa bei, mageuzi ya kiuchumi ili kuwa na uchumi jumuishi.

"Hizi ni fedha za masharti nafuu, zitasaidia kushusha bei ya mafuta, ruzuku ya pembejeo, kuwezesha vijana na makundi maalum. Haya ni matokeo ya dhamira njema ya serikali ya awamu ya sita, iko tayari kuendana na dunia," alisema.

Msigwa alisema pia ni matokeo ya ziara ya Rais Samia nchini Marekani, ambaye alikutana na viongozi mbalimbali ikiwamo IMF ambao walituma timu kuangalia mahitaji ya nchi na andiko lake, na kwamba walifanya tathmini na kuona nchi inastahili fedha hizo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa kwenye tovuti ya IMF, Bodi ya IMF imeidhinisha fedha hizo kati yake Dola za Marekani milioni 151.7 zitatolewa hivi karibuni.

Ilieleza kuwa fedha hizo ni kwa kipindi cha miezi 40 kwa ajili ya kutibu uchumi na kushughulikia makovu ya vita ya Ukraine na Russia, kusaidia utulivu kwenye uchumi wa watu wa kati, mageuzi ya kimuundo, ukuaji shirikishi na kuzingatia vipaumbele vya serikali.

IMF ilisema maboresho yanalenga kuimarisha nafasi ya kifedha kwa matumizi ya kijamii yanayohitajika, uwekezaji wa umma wenye matokeo mengi, kuanzisha upya mageuzi ya muundo wa mamlaka na kuimarisha na utulivu wa fedha nchini.

Katika taarifa hiyo, Naibu Mkurugenzi Mtendaji na Kaimu Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Bo Li, alisema Tanzania inaendelea kupona kutoka kwenye janga la UVIKO-19, ambalo lilizidisha changamoto za maendeleo na mageuzi ya kiuchumi katika kujenga uchumi imara.

Alisema fedha hizo zitatolewa kwa kuzingatia vipaumbele vya mpango mkakati wa miaka mitano wa Tanzania, na kwamba msaada wa IMF umelenga pia kuchochoea uwekezaji na ukuaji wa sekta binafsi na kuendelea kupata usaidizi kutoka kwa wadau wa maendeleo.

"Wakurugenzi Watendaji wameipongeza Tanzania kwa mwitikio wa kiuchumi kwenye janga la UVIKO-19 na sera zilizotungwa na kupunguza makali ya vita ya Ukraine. Makovu ya UVIKO -19 na vita vimeendelea kumomonyoa mafanikio ya kiuchumi yaliyopatikana kwa bidii," alisema na kuongeza:

"Kutokana na hali hii na kwa kuzingatia rekodi thabiti ya Tanzania katika utekelezaji wa mageuzi, Wakurugenzi waliunga mkono maombi ya nchi hiyo ili kukidhi mahitaji makubwa ya kifedha. Pia waliridhishwa na kasi ya utoaji chanjo za UVIKO-19."

Aidha, Bo Li, alisema IMF imeridhishwa na hatua za serikali kupunguza matumizi na kuelekeza nguvu kuboresha huduma za kijamii kwa ufanisi kwa wananchi.

Pia, namna nchi imeweka mkakati wa kukabiliana na kupanda kwa bei ya mafuta na chakula, ambayo itaangaliwa katika kuangalia uhimilivu wa deni.

Wakurugenzi hao walisisitiza umuhimu wa kuongeza uwekezaji na ukuaji wa sekta binafsi, kutekeleza ajenda ya mageuzi ya kiuchumi, uboreshaji rasilimali watu, usawa wa kijinsia, kuboresha takwimu za taifa na kushughulikia mabadiliko ya tabianchi.

## Kortini madai ya mauaji ya mjukuu

**Christina Haule,** MOROGORO

MKAZI wa Kidodi wilayani Kilosa, Shaibu Mkweche, amefikishwa katika Mahakama Kuu Kanda ya Morogoro kwa madai ya kumuua kwa makusudi mjukuu wake wenye miaka mitatu na mwili wake kukutwa umeharibika huku ukiwa hauna baadhi ya viungo.

Akisoma shtaka hilo, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Lilian Kombe, alidai mbele ya Jaji Paulo Ngwembe kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo Februari 10, 2021 katika kijiji na kata ya Kidodi kwa kumuua kwa makusudi Benedict Damas (3) baada ya kugombana na mke wake.

Kombe alidai kuwa Februari 9, 2021 mshtakiwa aligombana na mkewe, Pili Paulo, na kuanza kupigana, hivyo mkewe kuamua kuondoka na kwenda nyumba ya mbali kidogo ili kuepusha ugomvi huku akiwaacha watoto wake na mjukuu wake huyo ambaye kwa sasa ni marehemu.

Alidai kuwa siku iliyofuata, alirejea nyumbani na hakumkuta Benedict bali aliwakuta watoto wake na mumewe wakifunga mizigo kwa ajili ya kuhama na alipomuuliza aliko mjukuu wake, mumewe alidai hajui ndipo mwanamke huyo alipoamua kwenda kituo cha polisi kutoa taarifa ya kupotea kwa mtoto huyo.

Mwendesha mashtaka alidai kuwa Februari 24, 2021 mshtakiwa alikamatwa na polisi akiwa Mikumi na kukiri kuhusika na mauaji hayo kisha kuwapeleka polisi alipouacha mwili wa marehemu ambao ulikutwa eneo la Kidodi ukiwa umeshaanza kuharibika na hauna mikono. Alidai kuwa alipofikishwa polisi tena mbele ya askari wa upelelezi Koplo Nyakanyange, alikiri kuhusika na mauaji hayo.

Wakili wa Serikali, Evelyn Ndunguru, aliiomba mahakama kuendelea na shauri hilo kwa sababu ripoti ya afya ya akili ya mshtakiwa imesharudi kutoka hospitali ikionyesha kuwa yuko sawa kiakili.

Katika kuthibitisha mhusika kuhusika na mauaji hayo, Ndunguru alidai kuwa mashahidi 15 wanatarajiwa kutoa ushahidi wakati wa kusikiliza shauri hilo pamoja na vielelezo vinne.

Jaji Ngwembe alisema kesi hiyo itaendelea kusikilizwa huku mshtakiwa akitakiwa kubaki rumande hadi itakapotolewa hukumu kutokana na kesi ya mauaji ya kukusudia kutokuwa na dhamana.

Wakati huo huo, Joseph Mtangase na Rashidi Athumani wote wakazi wa Turiani wilayani Mvomero, wamepandishwa kizimbani katika mahakama hiyo wakikabiliwa na shtaka la kuua kwa kukusudia.

Mwendesha mashtaka Kombe alidai mahakamani hapo kuwa washtakiwa hao kwa pamoja Oktoba 29, 2019 kwa makusudi, huku wakijua kufanya hivyo ni kosa kisheria, walimuua Shabani Mwidini aliyekuwa akifanya kazi ya dereva wa bodaboda baada ya kumkodi kuwapeleka Turiani.

Katika kesi hiyo, Wakili Ndunguru alidai kuwa mashahidi 18 na vielelezo sita vitatumika katika kesi hiyo.

Jaji Ngwembe alisema jana alianza kusikiliza mashauri hayo kati ya 40 yaliyoko mezani kwake ambayo wataendelea kuyasikiliza hadi yanamalizika.

# Utata vifo watoto 5 wa familia moja

**Na Allan Isack,** MONDULI

UTATA umeibuka kutokana na vifo vya watoto watano wa familia moja katika Kijiji cha Mswakini, Monduli mkoani Arusha huku chanzo kikidaiwa kuwa chakula chenye sumu.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Frank Mwaisumbe, alithibitisha kutokea kwa tukio la watoto hao watano wa familia moja kupoteza maisha.

Mwaisumbe ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, humo, alisema inasadikika kuwa watoto hao walikula na kunywa kitu chenye sumu lakini bado haijajulikana aina ya sumu.

"Ni kweli kwamba kuna taarifa ya watoto watano kupoteza maisha na inasadikika walikula na kunywa kitu ambacho chenye sumu lakini bado haijathibitishwa ni aina gani ya sumu," alisema Mwaisumbe.

Alisema timu ya madaktari imekwenda katika familia hiyo na kuchukua sampuli ya sumu hiyo na kuipeleka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali jijini Dodoma kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

"Watoto hao watano wamefariki dunia baada ya kupewa maziwa na mama yao na kwa kuwa taarifa za tukio hilo zilifichwa, walicheleweshwa kupelekwa hospitalini, hivyo kusababisha kupoteza maisha," aliongeza.

Kadhalika, Mwaisumbe alisema wazazi wa watoto hao, wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa mahojiano zaidi na uchunguzi wa tukio hilo.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Mswakini, Nanga Karani, alisema watoto hao, walianza kuumwa kwa nyakati tofauti kuanzia Julai Mosi, mwaka huu.

Aliwataja watoto hao waliofariki dunia ni Bosii Nyangusi (14) mwanafunzi wa darasa la sita Shule ya Msingi Mswakini na Veronica Nyangusi(10) mwanafunzi wa darasa la tatu katika shule hiyo.

Wengine waliopoteza maisha ni pamoja na mapacha Faimaliye Nyangusi na Lemali Nyangusi (wote miaka minane) na Sophia Nyangusi (miaka sita).

"Wa kwanza kuanza kuumwa alikuwa Bosii na alipelekwa kupatiwa matibabu katika Hospitali ya FAME, iliyoko wilayani Karatu. Baadaye wenzake walianza kuumwa na walipelekwa kwenye hospitali ikiwamo Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru ambako mauti yaliwafika huko," alisema.

Mwenyekiti huyo, alithibitisha kushikiliwa kwa wazazi wote wawili wa marehemu na kwamba chunguzi wa tukio hilo bado unaendelea ili kufahamu chanzo halisi cha watoto hao kupoteza maisha.

Naye Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mount Meru, Dk. Kipapi Mlambo, alithibitisha kuwapokea wagonjwa wanne Julai 16, mwaka huu, na kwamba walipatiwa matibabu lakini hawakufanikiwa kuokoa maisha yao.

"Watoto wanne walifariki dunia hapa Mount Meru wakati wakipatiwa matibabu lakini taarifa za uchunguzi bado hazijatoka kama ni sumu walipewa au la kwa kuwa sampuli zimepelekwa kwa Mkemia Mkuu wa Serikali ili kuthibitisha kama ni sumu. Kwa sasa ni ngumu kuthibitisha hadi tutakapopata taarifa kutoka kwa mkemia mkuu.

"Hadi sasa uchunguzi umefanyika kwa maiti tatu za waliofariki dunia hapa hospitalini na sampuli zimeshapelekwa. Kilichobaki ni kufuatilia majibu kufahamu chanzo halisi cha tukio hilo," alisema.



Mkurugenzi Mkuu wa Global Education Link (GEL), Abdulmalik Mollel, akifafanua jambo kwa baadhi ya wananchi waliotembelea banda lake, kujua masuala mbalimbali ya vyuo vikuu vya nje ya nchi vilivyoko kwenye maonyesho ya vyuo vikuu kwa mwamvuli wa GEL, katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. Habari Uk. 10. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mume na mke kortini mashtaka kukutwa na meno 413 ya tembo

**Na Grace Gurisha**

MKAZI wa Chamanzi, Abdul Abdallah (35) na mkewe, Salma Mshamu (21) wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu wakikabiliwa na mashtaka ya kukutwa na meno ya tembo 413 yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni nne.

Washtakiwa hao pia wanadaiwa kukutwa na meno mawili ya kiboko yenye thamani ya Sh. milioni 3.453 kinyume cha Sheria ya Wanyamapori.

Akisoma hati ya mashtaka mahakamani huko jana, Wakili Mwandamizi Timotheo Mmari, alidai mbele ya Hakimu Mkazi, Pamela Mazengo, kuwa washtakiwa wanatuhumiwa kwa mashtaka matatu ya kujihusisha na biashara ya nyara za serikali na mawili ya kukutwa na nyara za serikali.

Alidai kati ya Januari Mosi, 2017 na Septemba 3, 2019 maeneo ya Saku Chamanzi ndani ya Wilaya ya Temeke, Dar es Salaam, washtakiwa wote kwa pamoja walinunua na kupokea meno ya tembo 413.

Inadaiwa kwamba meno hao yana thamani ya Dola za Marekani 1,755,000 sawa na Sh. 4,040,010,000 pamoja na meno mawili ya kiboko yenye thamani ya Dola za Marekani 1,500 sawa na Sh. 3,453,000.

Mmari alidai kwamba katika shtaka la pili, tarehe hiyo hiyo, wote kwa pamoja, maeneo ya Saku Chamanzi, Wilaya ya Temeke, walikutwa na meno hayo ambayo ni mali ya Serikali ya Tanzania bila kuwa na kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori.

Alidai katika shtaka la tatu, tarehe hiyo na maeneo hayo, washtakiwa wote kwa pamoja walikutwa na meno mawili ya kiboko yenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni tatu, mali ya Tanzania bila ya kuwa na kibali kutoka kwa mkurugenzi wa wanyamapori.

Mmari alidai upelelezi wa shtaka hilo umekamilika na wanasubiri kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) aridhie shauri hilo liendelee mahakamani huko.

Hakimu Mazengo alisema mahakama hiyo haina uwezo wa kusikiliza shauri hilo kwa kuwa ni la uhujumu uchumi na baada ya uchunguzi kukamilika, litapelekwa katika Mahakama ya Mafisadi.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Agosti 2, 2022 kwa ajili ya kutajwa.

# Majaliwa aagiza ufuatiliaji wa mafunzo Watanzania ughaibuni

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa ameitaka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuendelea kusimamia na kufanya ufuatiliaji wa karibu zaidi mwenendo wa baadhi ya asasi zinazosajili na kuratibu wanafunzi wanaokwenda kusoma vyuo vikuu nje ili kukidhi viwango vinavyotakiwa.

Ameelekeza vyuo wanavyopaswa kupelekwa Watanzania, viwe na mafunzo yatakayomletea Mtanzania manufaa na yanayotambuliwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU).

Majaliwa aliagiza hayo jana jijini Dar es Salaam alipofungua maonyesho ya 17 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia yanayoendelea kwenye Viwanja vya Mnazi Mmoja, yakiratibiwa na TCU.

Maonyesho hayo yamebebwa na kaulimbiu 'Elimu ya Juu Inayokidhi Mahitaji ya Soko la Ajira kwa Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi'.

Alisema Julai 26, 2017 alishiriki maonyesho kama hayo viwanjani huko, akikumbusha kuwa pamoja na mambo mengine, alipata malalamiko mengi kuhusu mifumo yote ya elimu kwa sekta binafsi na umma.

Alisema alielekeza kusimamia kwa ukaribu taratibu zote zinazofanywa na asasi na kampuni zinazojishughulisha na uratibu wa wanafunzi wanaokwenda kusoma nje ya nchi.

"Matatizo makubwa wakati ule yalikuwa ni kutotambulika kwa baadhi ya vyuo vya nje wanakosoma vijana wetu, hata mafunzo yanayosomwa kwenye baadhi ya vyuo huko nje na kusababisha usumbufu kwa vijana wanapomaliza masomo yao.

"Kupoteza fedha kwa kusoma masomo kwenye vyuo visivyotambulika na baada ya kumaliza anakuwa hatambuliki pia na vigezo vya kimataifa kupitia taasisi ya TCU. Ninafurahi marekebisho yamefanywa na hatujapata malalamiko mengi kama ilivyokuwa mwaka 2017," alisema.

Majaliwa alisema hiyo ina maana Wizara ya Elimu na TCU wametekeleza maelekezo kwa kiwango cha kuridhisha.

Alitoa wito kwa Wizara ya Elimu kuendelea kusimamia na kufanya ufuatiliaji wa karibu zaidi kuhusu mwenendo wa baadhi ya asasi zinazosajili na kuratibu wanafunzi wanaokwenda kusoma vyuo vikuu vya nje ya nchi.

"Tunayasema haya kwa sababu taasisi zetu zinazosaidia kupata vyuo vya nje, nazo zinafanya biashara. Anaweza akawa anapata fedha tu lakini asiangalie ubora wa chuo na mafunzo wanayokwenda kusoma vijana.

"Lengo letu ni kuhakikisha kwamba asasi au kampuni husika zinasajiliwa na kukidhi vigezo, zitoe miongozo mizuri kwa vijana na vijana wanapokwenda, wajue wanakwenda kusoma mafunzo ambayo yanatambuliwa na TCU. Walioomba kwenda kusoma nje, ni vizuri wachanje ili wasipate usumbufu," aliagiza.

Kuhusu kaulimbiu ya mwaka huu, Majaliwa alisema inaleta changamoto kwa taasisi za elimu ya juu kuhakikisha zinatoa maarifa na ujuzi unaotakiwa katika soko la ajira.

"Mwaka 2014 serikali kupitia iliyokuwa Tume ya Mipango, ilifanya tathmini ya hali ya soko la ajira na ujuzi unaotolewa ili kuwa na uchumi imara na shindani ifikapo mwaka 2023, yaani miaka miwili kabla ya ukomo wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Taifa ya Juni 1999 hadi 2025.

"Tathmini hii ilibainisha viwango vya ujuzi na wanaotafuta ajira, vipo chini ya kiwango kinachohitajika kwa waajiri. Baadhi ya upungufu uliobainishwa, ni uwezo mdogo, wahitimu kushindwa kujiamini, kukosa ubunifu na kutojituma kutatua matatizo," alisema.

Katibu Mtendaji wa TCU, Prof. Charles Kihampa, alisema katika maonyesho hayo ya 17, jumla ya taasisi 75 zimeshiriki, ikiwa ni ongezeko la taasisi moja kulinganisha na taasisi 74 zilizoshiriki maonyesho hayo mwaka jana.

Mwenyekiti wa TCU, Prof. Penina Mlama, alisema tume imekuwa ikiandaa maonyesho hayo kwa lengo la kutangaza huduma, kuimarisha uhusiano baina ya taasisi za elimu ya juu na wananchi ambao hufika kujionea shughuli mbalimbali zinazofanywa ikiwamo kushiriki kuomba nafasi za masomo ndani na nje ya nchi.

Prof. Mlama aliihakikishia serikali kuwa TCU itaendelea kuwa imara katika kusimamia kudhibiti ubora wa elimu ya juu ili iwe chachu kwa maendeleo ya nchi na kuzalisha wahitimu ambao watakuwa washindani katika soko la ajira.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kushoto), akimsikiliza mwandishi wa kitabu kiitwacho Kipenga cha Mwisho kilichoandikwa na Bernadeta Msigwa wa Chuo Kikuu Huria, katika maonyesho ya 17 ya vyuo vikuu vya Tanzania, viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Serikali yatangaza neema kwa vijana

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI inatarajia kujenga vituo atamizi vya vijana kwenye kanda tano nchini huku ikipanua wigo wa mafunzo ya ujuzi kwa ajili ya kujenga uchumi wa buluu kwenye maeneo ya Ziwa Victoria, Tanganyika na Bahari ya Hindi

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na wanafunzi wa vyuo vya ufundi vya Don Bosco na VETA jijini hapo ambao wananufaika na programu ya kukuza ujuzi kitaifa inayotekelezwa na ofisi hiyo.

Alisema vituo hivyo vitajengwa kwa mwaka wa fedha 2022/23 na vitatumika kulea vijana wenye ujuzi.

"Kwa mfano ukimaliza mafunzo yako ukitaka kusindika chakula kutakuwa na vifaa ambavyo vinaweza kutumika na itaongeza fursa kwa vijana hasa wasio na uwezo wa kununua vifaa vya kusindika au kufanya shughuli unayofanya," alisema.

Kuhusu wigo wa mafunzo, Prof. Ndalichako alisema kumekuwapo na kilio kikubwa hasa kwa vijana wanaotoka maeneo yenye bahari na maziwa na kwamba mafunzo yanayotolewa hayajawazingatia.

"Kwa mwaka wa fedha 2022/23 sasa tunataka kutoa mafunzo kwa vijana kwa ajili ya kujenga ujuzi wa uchumi wa buluu, kama kuwawezesha kupata mafunzo ya ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba, ili kuongeza ufanisi," alisema.

Pia alisema kuongeza thamani ya samaki kwa kukausha samaki na dagaa ambapo wamekuwa wakikaushwa kwenye mchanga na hivyo kuwa na mchanga.

"Kwa mfano kule Mwanza tumeambiwa kunahitajika teknolojia ya ukaushaji dagaa kutokana na kukaushiwa kwenye mchanga na hivyo kukosa ubora," alisema.

Aidha, alisema kupitia programu hiyo ya mafunzo ya uanagenzi na uzoefu kazini kwa mwaka wa fedha 2021/22, vijana 22,200 wamepata mafunzo.

"Katika mafunzo ya uzoefu kazini kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni, 2022, vijana 2,246 wamepata mafunzo hayo, na wengine hupata fursa ya kuajiriwa huko wanapofanya mafunzo," alisema.

Pia alisema vijana 2,644 wamerasimishiwa ujuzi ambao walipata ujuzi kupitia mfumo usio rasmi.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, aliwataka vijana hao kuthamini jitihada zinazofanywa na serikali ya kuwakwamua kiuchumi kwa kutoa mafunzo bure ya ujuzi.

Awali, Mkuu wa Chuo cha Ufundi cha Don Bosco, Padri Boniphace Mchami, alisema programu hiyo imewawezesha vijana kupata ujuzi wa fani mbalimbali zitakazosaidia kujiajiri na kuajiriwa.

# Mradi wa mabilioni kumaliza kero maji

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

SERIKALI kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) imetia saini mkataba wa Euro milioni mbili na kampuni ya SEURECA Consulting Engineering ya Ufaransa itakayoshirikiana na Kampuni ya NETWAS ya Tanzania kufanya upembuzi yakinifu, usanifu na usimamizi wa ujenzi wa mradi wa miundombinu ya kupeleka maji maeneo ya kusini mwa Jiji la Mwanza.

Akizungumza wakati wa kutia saini mkataba jijini Mwanza juzi, Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Mhandisi Leonard Msenyele, alisema mkataba huo ni hatua za awali za utekelezaji wa mradi wa kufikisha huduma ya maji kwenye maeneo ya wilaya za Nyamagana, Misungwi na Magu.

Kwa wilaya ya Nyamagana, Mhandisi Msenyele alitaja maeneo yatakayonufaika kuwa ni Buhongwa, Nyamazobe, Sahwa, Lwanhima, Fumagila, na Kishiri wakati kwa Wilaya ya Misungwi, maeneo ya Usagara, Nyashishi, Nyang'homango, Kigogo Ferry, Bujingwa na Fella yatanufaika. Maeneo yatakayonufaika kwa wilaya ya Magu ni Kisesa, Bujora, Isangijo, Kanyama, Igekemaja na Ihayabuyaga.

Alisema mkataba huo umegawanyika katika sehemu mbili, ya kwanza ikiwa ni kufanya upembuzi yakinifu, tathmini ya athari za mazingira na kijamii na usanifu na sehemu ya pili ni kumsimamia mkandarasi atakayetekeleza mradi huo.

Mhandisi Msenyele alibainisha kuwa uhitaji wa huduma ya maji kwenye maeneo hayo ni mkubwa na kwamba wananchi wanayo matarajio makubwa na mradi huo kutokana na baadhi ya maeneo hadi sasa kutokuwa na mtandao wa maji safi.

"Kuna uhitaji mkubwa wa huduma ya maji kwenye maeneo haya, ni matumaini yangu kwamba kutokana na uzoefu wenu mtafanya kazi kwa mujibu wa mkataba. Wananchi wanahitaji maji, hawataki kutusikia tukizungumzia habari za michakato," alisisitiza.

Alizihakikishia kuzipa ushirikiano wa karibu kampuni hizo na alizielekeza kuanza shughuli mara moja ili mapema mwakani, ujenzi wa mradi uanze ikiwamo ujenzi wa vituo vinne vya kusukuma maji, ujenzi wa matangi manne ya ujazo tofauti ya kuhifadhia maji, uchimbaji wa mitaro na ulazaji wa mabomba ya kusambazia maji yenye urefu wa takriban kilomita 400.

Mhandisi Mshauri wa SEURECA Afrika Mashariki, Christophe Lacarin, aliihakikishia serikali kuwa watakamilisha kazi ya mradi kwa wakati na kwa ubora mkubwa kulingana na uzoefu wa muda mrefu walio nao kwenye shughuli za usanifu na usimamizi wa miradi.

"Tunauhitaji huu mradi, tuna imani kwa ubora wa kazi zetu mradi huu utatuletea miradi mingine mingi na tumetekeleza miradi mingi maeneo mbalimbali duniani ambayo inaendelea kutengenezea mazingira ya kupata kazi," alisema Lacarin.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi MWAUWASA, Poas Kilangi, alisema mkataba huo ni wa miezi 44 na utekelezaji wake unapaswa kuanza ndani ya siku 28 kutoka siku ya utiaji saini.

**TANGAZO**

# TAARIFA YA VIWANGO VYA TIGO KWA ROBO YA PILI (APRILI - JUNI 2022)

## Viwango unavyotozwa kwa kadri unavyotumia (Na Kodi)

** - Malipo ya sauti yamekadiriwa kwenye sekunde iliyo karibu
- Malipo ya data yamekadiriwa kwa shilingi 0.1 kwa kila kilobaiti 10 za data

**VIWANGO VYA NDANI**

| Aina za simu | Bei (TSh/Dk) |
|---|---|
| Tigo - Tigo (Viwango ni vya muda wowote) | 30 |
| Tigo - Mitandao mingine (Viwango ni vya muda wowote) | 30 |

**VIWANGO VYA KIMATAIFA**

| Aina za simu (Kanda/Makundi) | Bei (TSh/Dk) | Nchi |
|---|---|---|
| Kundi 1 | 720 | China, India, Marekani, Canada, USA, Canada |
| Kundi 2 | 1020 | Kenya, Angola, Afrika Kusini, Nigeria, Botswana, Ghana, Ethiopia |
| Kundi 3 | 1020 | Lebanon, Israeli, Hispania, U.A.E, Uingereza (simu za kiganjani), Uingereza (Simu za mezani) |
| Kundi 4 | 1200 | Sweden, Hong Kong, Pakistani, Yemen, Ufilipino, Saudi Arabia, Uholanzi, Japan, Malaysia, Norway, Ireland, Pakistan, Yemen, Phillipines, Saudi Arabia, Netherlands, Japan, Malaysia, Norway, Ireland |
| Kundi 5 | 1800 | Australia, Nepal, Uturuki, Urusi, Visiwa vya Comoro, Uganda, Rwanda, Ufaransa, Denmark, Italia, Oman, Ujerumani |
| Kundi 6 | 2520 | Nchi nyinginezo |
| Kundi 7 | 2520 | Cuba, DRC, Burundi, Zimbabwe, Msumbiji, Uswisi, Malawi, Zambia, Burundi, Zimbabwe, Mozambique, Switzerland, Malawi, Zambia |
| Kundi 8 | 19800 | Mitandao yote ya satelaiti |

**VIWANGO VYA SMS**

| Aina za SMS | Bei (TSh/SMS) |
|---|---|
| SMS za kitaifa | 8 |
| SMS za kimataifa | 215 |

**DATA TARIFFS**

| Intaneti | Bei (TSh) |
|---|---|
| Data kwa MB | 9.35 |

## VIWANGO VYA VIFURUSHI VYA DAKIKA, INTANETI NA SMS (Na Kodi)

**MITANDAO YOTE**

| Bei (TSh) | Jumla ya Dakika | Dakika za Tigo - Tigo | SMS | MB | Muda |
|---|---|---|---|---|---|
| 500 | 100 | 90 | 25 | 0 | Saa 24 |
| 500 | 30 | 0 | 15 | 0 | Saa 24 |
| 500 | 30 | 0 | 20 | 5 | Saa 24 |
| 2000 | 150 | 50 | 150 | 700 | Saa 24 |
| 1000 | 310 | 270 | 25 | 0 | Saa 48 |
| 1000 | 150 | 0 | 50 | 20 | Saa 48 |
| 1000 | 150 | 0 | 25 | 0 | Saa 48 |
| 1500 | 300 | 250 | 30 | 0 | Siku 7 |
| 1500 | 150 | 0 | 20 | 0 | Siku 7 |
| 1500 | 250 | 0 | 100 | 0 | Siku 7 |
| 2000 | 250 | 0 | 100 | 50 | Siku 7 |
| 3000 | 400 | 0 | 50 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | 700 | 0 | 50 | 0 | Siku 7 |
| 3000 | 270 | 200 | 100 | 1024 | Siku 7 |
| 5000 | 450 | 250 | 250 | 1536 | Siku 7 |
| 10000 | 1100 | 0 | 100 | 150 | Siku 7 |
| 5000 | 300 | 0 | 50 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | 300 | 0 | 200 | 5120 | Siku 30 |
| 10000 | 1200 | 0 | 50 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | 1200 | 0 | 200 | 200 | Siku 30 |
| 20000 | 2700 | 0 | 200 | 200 | Siku 30 |
| 20000 | 3000 | 0 | 100 | 0 | Siku 30 |
| 30000 | 3300 | 0 | 100 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | 750 | 150 | 500 | 2560 | Siku 30 |
| 20000 | 1600 | 300 | 500 | 7168 | Siku 30 |
| 30000 | 1500 | 300 | 500 | 14336 | Siku 30 |
| 50000 | 2900 | 400 | 500 | 23552 | Siku 30 |

**KIMATAIFA**

| Bei (TSh) | Jumla ya Dakika | SMS | MB | Muda |
|---|---|---|---|---|
| 1000 | India, Marekani, Canada, China - Dk 10 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | India, Marekani, Canada, China - Dk 40 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Uingereza (+441, +442), Ujerumani, Ireland, Norway - Dk 5 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Kenya, Rwanda, Angola, Afrika Kusini, Nigeria - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 5000 | Uganda, Malawi, Burundi, Moroko, Algeria - Dk 3 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 3000 | Omani, UAE, Yemen, Pakistan, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon - Dk 4 | 0 | 0 | Saa 24 |
| 6000 | Kenya, Rwanda, Angola, Afrika Kusini, Nigeria - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Uganda, Malawi, Burundi, Moroko, Algeria - Dk 6 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | Ufaransa - Dk 4 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | India, Marekani, Canada, China - Dk 80 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Uingereza (+441, +442), Ujerumani, Ireland, Norway - Dk 12 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 5000 | Omani, UAE, Yemen, Pakistan, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 7 |
| 10000 | Kenya, Rwanda, Angola, Afrika Kusini, Nigeria - Dk 14 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 15000 | Uganda, Malawi, Burundi, Moroko, Algeria - Dk 10 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Kenya, Rwanda, Angola, Afrika Kusini, Nigeria - Dk 29 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 22000 | Uganda, Malawi, Burundi, Moroko, Algeria - Dk 15 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | India, Marekani, Canada, China - Dk 180 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 15000 | Ufaransa - Dk 13 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Uingereza (+441, +442), Ujerumani, Ireland, Norway - Dk 24 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 10000 | Omani, UAE, Yemen, Pakistan, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon - Dk 18 | 0 | 0 | Siku 30 |
| 20000 | Omani, UAE, Yemen, Pakistan, Saudi Arabia, Qatar, Lebanon - Dk 8 | 0 | 0 | Siku 30 |

**SMS**

| Bei (TSh) | Jumla ya Dakika | SMS | MB | Muda |
|---|---|---|---|---|
| 500 | 0 | 500 | 0 | Saa 24 |
| 1000 | 0 | 5000 | 0 | Siku 7 |
| 2000 | 0 | 10000 | 0 | Siku 30 |

**BILA KIKOMO**

| Bei (TSh) | Jumla ya Dakika | SMS | MB |
|---|---|---|---|
| 500 | 6 | 0 | 0 |
| 1000 | 30 | 0 | 0 |
| 2000 | 45 | 0 | 0 |
| 1000 | 0 | 0 | 150 |

**INTANETI**

| Bei (TSh) | MB | Muda | Ziada |
|---|---|---|---|
| 500 | 150 | Saa 24 | N/A |
| 1000 | 650 | Saa 24 | N/A |
| 2000 | 1331 | Saa 24 | N/A |
| 1000 | 650 | Siku 3 | N/A |
| 2500 | 1638 | Siku 3 | N/A |
| 2000 | 1024 | Siku 7 | N/A |
| 3000 | 1741 | Siku 7 | N/A |
| 5000 | 3072 | Siku 7 | N/A |
| 10000 | 6144 | Siku 7 | N/A |
| 15000 | 9728 | Siku 7 | N/A |
| 3000 | 1843 | Siku 30 | N/A |
| 10000 | 5120 | Siku 30 | N/A |
| 20000 | 12288 | Siku 30 | N/A |
| 35000 | 22528 | Siku 30 | N/A |
| 50000 | 32768 | Siku 30 | N/A |

**MIC TANZANIA PLC,**
Derm Complex, Kiwanja Namba 11, Kitalu 45 A, Barabara ya Bagamoyo
S.L.P 2929, Dar es Salaam, Tanzania.

**www.tigo.co.tz**

tigo

216950302

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Shime tujiandae kuhesabiwa kwa maendeleo

**WAKATI** elimu na uhamasishaji wa wananchi kushiriki Sensa ya Watu na Makazi, inayotarajiwa kuanza Agosti 23, mwaka huu, ikiendelea jamii imetakiwa kujijengea uelewa wa umuhimu wa siku hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Mtakwimu ya Taifa (NBS), kwenye tovuti yake, utekelezaji wa sensa utafanyika kwa awamu tatu ambazo ni kabla ya kuhesabu, wakati wa kuhesabu na baada ya kuhesabu watu.

Kipindi cha kabla ya kuhesabu watu kinajumuisha mambo mbalimbali, ikiwamo uandaaji wa kitabu cha mkakati wa usimamizi na utekelezaji wa sensa na nyaraka nyingine.

Pia, utengaji wa maeneo ya kuhesabia na uzalishaji wa ramani na uandaaji wa madodoso na miongozo mbalimbali na uhamasishaji.

Baada ya kuhesabu watu kinajumuisha uchakataji wa taarifa za sensa, uchambuzi, utoaji wa matokeo ya awali, usambazaji wa matokeo ya mwisho, uhamasishaji wa matumizi ya takwimu kwa watumishi wa wizara, Idara na taasisi za serikali.

Elimu ya sensa inatolewa ili jamii ifahamu umuhimu wa kutoa ushirikiano kwa makarani watakaokuwa wamepewa kazi ya kuchukua taarifa muhimu.

Uhamamishaji huo unazingatia kuitaka jamii kutoa taarifa zitakazowezesha serikali kupanga mipango yake ya maendeleo kwa ajili ya wananchi wake.

Bila kuwa na takwimu sahihi ya idadi ya watu ni vigumu serikali kupanga bajeti itakayotosheleza mahitaji ya wananchi wake kuanzia kwenye sekta ya afya, elimu na huduma muhimu za maji na umeme.

Idadi ya watu ndiyo mwongozo utakaowezesha serikali kutambua katika kuleta maendeleo inajipanga vipi kutokana na idadi hiyo.

Ni lazima makundi yote ya watu yajulikane kuanzia wazee, vijana, watoto, wanawake na wanaume ili kutoa picha nzuri itakayoongoza katika mipango hiyo.

Kuna baadhi ya watu wamekuwa wakificha kundi fulani likiwamo la wenye ulemavu na kulikosha haki ya kunufaika na mipango ya serikali.

Watoto wenye ulemavu wamekuwa wakikosa haki yao ya kupata elimu kutokana na baadhi ya wazazi kuwaficha ndani ili wasitambulike kwenye jamii.

Hali hii imesababisha watoto hao kusoma misaada mbalimbali ikiwamo ya vifaa vya kuwawezesha kurahisisha maisha yao.

Katika kuhakikisha uchukuaji taarifa za sensa unakwenda vizuri, makarani watakaoteuliwa kufanyakazi hiyo ni lazima wajue jinsi ya kutumia lugha nzuri wanapokwenda kwa wananchi.

Wengine hugoma kutoa taarifa zao kwa sababu tu hakuongozwa vizuri kwa lugha itakayomfanya mtu atoe ushirikiano bila kikwazo.

Wasimamizi wa sensa pia wanatakiwa kuwa waadilifu kwa kutunza siri zitakazotolewa na wananchi kwani hiyo pia ni changamoto inayofanya watu washindwe kutoa taarifa zao kwa kuogopa taarifa zao kusambazwa kusikostahili.

Serikali imetumia gharama kubwa kuhakikisha zoezi hilo linakwenda vizuri, kuanzia kwenye vifaa vitakavyotumika hadi kwa watu watakaochukuliwa kufanya kazi hiyo.

Ni vizuri basi lengo hilo ambalo serikali imejiwekea kwa ajili ya kuleta maendeleo ya wananchi wake, lisiharibiwe na watu wachache.

Kwa ushirikiano hakuna jambo litakaloshindikana na maendeleo yatapatikana kwa wote.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Miaka 30 ya vyama viongozi watafakari wanakwama wapi

Na Sabato Kasika

**BAADA** ya mfumo wa vyama vingi vya siasa kurejeshwa nchini mwaka 1992, baadhi ya wanasiasa wenye nia ya mageuzi ya kisiasa, walijitokeza haraka na kuanzisha vyama hivyo kwa wingi.

Wingi huo wa vyama, ulisababisha serikali kufikiria kuvipunguza, lakini Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere akasema hata vikiwa vingi kama utitiri ni sawa na kutaka viachwe, huku akiamini kwamba vingeweza kujifia vyenyewe.

Kwa sasa ni wazi utabiri wa Baba wa Taifa ulishatumia, kutokana na ukweli kwamba vipo ambavyo vilifutika vyenyewe bila kuguswa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, vipo vilivyofutwa na vingine vinaendelea kusuasua.

Ukweli ni kwamba umri wa miaka 30 tangu kurejeshwa kwa mfumo huo, ni mkubwa vilitakuwa kuwa vimeshakomaa na kuwa na uwezo wa kujiendesha, kwa kuwa miradi mingi na ofisi zake.

Lakini bahati mbaya, vingi ni kama havipo na vimebaki kusubiri kuibuka wakati wa uchaguzi na kukodi vyumba na kuvifanya kuwa ofisi za muda uchaguzi ukiisha, navyo vinarudi 'mafichoni'.

Kwa utaratibu kama huo, havitwezi kufika mbali, kwa sababu si rahisi viongozi wake kushawishi watu wakajiunga navyo na badala yake vinakuwa vinasindikiza vingine kana kwamba havina malengo.

Pengine ni wakati wa kutafakari walikojikwaa na kusababisha kuyumba ili kuchukua hatua. Kuna sababu mbalimbali ambazo zimekuwa zikitajwa na wadau wa siasa kuwa zinachangia vyama kuyumba, kubwa ikiwa ni wanachama na viongozi wake kutofautiana kimawazo, kimtazamo na hatimaye kuzusha migogoro.

NCCR-Mageuzi ni miongoni mwa vyama vinavyokabiliwa na mzozo wa uongozi kwa sasa, ambao haujapata ufumbuzi.

Hatima ya migogoro hiyo huwa ni kufukuzana bila kujali kwamba, kila mtu ana mapungufu yake na pia suala la kutofautiana kimtazamo au kimawazo ni la kawaida na linaweza kusaidia kujenga chama.

> **Si vyema kuendekeza migogoro na kufurahia kufukuzwa kwa baadhi ya wanachama, kwani mtindo huo unachangia kudhoofisha vyama na kubaki vimedumaa kwa kukosa wanachama na wafuasi.**

Sidhani katika wingi wa watu wanaweza kuwa na mawazo au mtazamo wa kufanana, lakini utofauti ndizo ambazo zinaweza kusaidia kuimarisha chama iwapo kila mmoja atapewa nafasi ya kuelezea mtazamo au mawazo yake.

Ikitokea katika wingi huo watu kila jambo linakuwa ni ndiyo kila wakati bila kuhoji, ni wazi kutakuwa na sehemu ambayo haiko sawa, aidha kwa wanachama au kwa viongozi wa chama husika.

Hivyo, ni nafasi kwa viongozi wa vyama kutafakari kwa kina wakitambua kuwa miaka 30 ambayo vimekuwapo ni mingi, inatosha kuvifanya viwe imara badala ya kuonekana kama vilianzishwa juzi.

Ikumbukwe kuwa, chama ni wanachama, bila wanachama hakuna chama, hivyo, ni muhimu viwe na mpango mkakati wa kuhakikisha vinakuwa na wanachama wa kutosha watakaoviwezesha kushika dola.

Si vyema kuendekeza migogoro na kufurahia kufukuzwa kwa baadhi ya wanachama, kwani mtindo huo unachangia kudhoofisha vyama na kubaki vimedumaa kwa kukosa wanachama na wafuasi.

Uimara wa chama unategemea ukomavu wa kisiasa walionao viongozi na jinsi ya uendeshaji wa chama katika katika dhana na misingi ya demokrasia, uwazi katika ushiriki wa wanachama kukitumikia na kufanya maamuzi muhimu.

Kutofautiana kimtazamo, kimawazo ni jambo la kawaida, hivyo lisingefaa kuchukuliwa kama usaliti na kufikia kuzusha migogoro katika vyama, badala yake iwe ni fursa ya kujirekebisha.

Tanzania na vyama imara vya siasa visivyo na migogoro na vyenye malengo ya kushika dola inawezekana, iwapo kutakuwa na dhamira ya kweli, ni viongozi wenyewe wa vyama kutafakari na kuchukua hatua sahihi.

## Vituo 19 kujengwa kudhibiti wanyama waharibifu

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SERIKALI inakusudia kujenga vituo 19 vya kambi za askari kwa mwaka wa fedha 2022/23 ili kukabiliana na uharibifu wa mazao ya wananchi unaofanywa na wanyamapori wakali.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, alisema hayo jana jijini hapo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu vipaumbele vya wizara hiyo kwa bajeti ya 2022/23.

Alisema hatua hiyo imetokana na kuwapo kwa matukio mengi ya wanyamapori hao kufanya uharibifu wa mazao ya wananchi.

Pia alisema Wizara itatoa elimu juu ya mbinu rafiki za kukabiliana na migogoro baina ya binadamu na wanyamapori wakali na kuwawezesha vitendea kazi vya kukabiliana nao.

Alisema wizara hiyo itaendelea na kushirikiana na wananchi hao wanaoishi jirani na maeneo ya hifadhi pamoja na wizara zingine za kisekta ili kuweka mipango bora ya matumizi ya ardhi ya vijiji kwa lengo la kuepusha migongano.

Kadhalika, alisema Wizara itaanza matumizi ya mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kupokea taarifa za kifuta jasho ambacho ni pole ambayo inatolewa kwa wananchi kutokana na madhara yaliyosababishwa na wanyamapori hao.

Kuhusu filamu ya kutangaza utalii ya The Royal Tour, alisema wanaendelea kutangaza utalii kitaifa na kimataifa kwa kuibua masoko mapya ya utalii ili kuongeza idadi ya watalii.

Pia alisema katika kuboresha huduma za malazi na chakula nchini kwa mwaka 2022/23 Wizara itaanza kutumia mfumo wa kielektroniki wa kupanga huduma hizo katika madaraja ya ubora wa nyota.

Dk. Chana alisema katika kuendeleza kampeni za kutunza mazingira Wizara itaandaa mipango ya usimamizi wa misitu 57 yenye ukubwa wa hekta 1,703,202 na kufanya mapitio ya usimamizi wa misitu ya hifadhi 111 pamoja na kuhakiki kupima mipaka ya misitu 133 na yenye urefu wa kilomita 33,107.

Alisema katika bajeti hiyo wanakusudia kukarabati, kuimarisha na kujenga miundombinu ya barabara, madaraja katika maeneo ya hifadhi na kuboresha mifumo ya mawasiliano ili kuwavutia watalii.

# Miradi 129 kichefuchefu yaanza kutoa maji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MIRADI ya maji 129 iliyobainika kuwa kichefuchefu imerekebishwa na kuanza kutoa huduma kwa wananchi huku 48 ikitarajiwa kukamilika Desemba, mwaka huu.

Aidha, zaidi ya watu milioni 2.5 wamenufaika na huduma ya majisafi kwa mwaka wa fedha 2021/22 kupitia miradi iliyotekelezwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA).

Akizungumza jana na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa majukumu ya wakala na mwelekeo wa bajeti ya 2022/23, Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA, Clement Kivegalo, alisema wakati wakala unaanza kazi, ulikabidhiwa miradi 177 ambayo ilikuwa imekamilika lakini haitoi maji na kwa sasa miradi 129 imerekebishwa.

Kivegalo alisema kwa mwaka 2021/22, RUWASA imeokoa Sh. bilioni 57.4 kupitia majadiliano ya kina ya mikataba na makandarasi kwa miradi 86 baada ya kubaini inatekelezwa kwa gharama kubwa.

"Kupitia majadiliano hayo, RUWASA iliokoa Sh. bilioni 57.4 kabla ya majadiliano, gharama kwa miradi yote 86 ilikuwa Sh. bilioni 367.3 na baada ya majadiliano, gharama ilipungua hadi Sh. bilioni 309.9," alisema.

**BEI MAJI VIJIJINI**

Alisema bei ukomo za maji vijijini zilizotangazwa mwishoni mwa mwezi Juni, 2022, zitaanza kutumika Agosti mwaka huu.

"RUWASA ilitangaza bei ukomo za maji ambao umelenga kutatua bei kubwa ya maji. Kwa mfano kabla ya kutangazwa kwa bei ukomo, ndoo moja ya maji ya lita 20 ilikuwa inauzwa kwa Sh. 100 kwa miradi zinazotumia dizeli. Baada ya bei ukomo kutangazwa, bei ya ndoo moja ya lita 20 ilishuka kutoka Sh. 100 hadi kufika Sh.50," alisema. Mkurugenzi huyo alisema katika kuhakikisha kuwa gharama za uendeshaji wa miradi zinapungua na huduma inakuwa endelevu, RUWASA inashirikiana na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na REA kubadilisha mifumo ya nishati ya uendeshaji wa mitambo ya maji kutoka kwenye mfumo wa dizeli kwenda mfumo wa umeme jua na wa TANESCO.

"Hadi sasa, miradi 19 kati ya 74 za mikoa miwili ya Singida na Dodoma tayari imebadilishwa kwa kufungwa umemejua na kazi hii itaendelea kwa awamu kwa nchi nzima,"alisema.

**UTEKELEZAJI MIRADI**

Kivegalo alisema kwa mwaka huo wakala huo ulipanga kutekeleza miradi ya maji 1,527, ambapo kati ya hiyo miradi 873 ilikuwa inaendelea na utekelezaji huku 303 imekamilika.

Hata hivyo, alisema miradi 225 kati ya miradi iliyokuwa inaendelea na utekelezaji inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Septemba, mwaka huu na miradi 648 itaendelea na utekelezaji na itawezesha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi 1,467,107 kupitia vituo vya kuchotea maji 4,147 vilivyojengwa katika maeneo ya vijiji mbalimbali.

**MIRADI YA UVIKO-19**

Kuhusu miradi ya UVIKO- 19, Kivegalo alisema serikali ilitoa fedha ya nyongeza ya Sh.bilioni 78.53 kupitia kupitia fedha za UVIKO- 19 kwa ajili ya kutekeleza miradi 172 ya maji vijijini ambapo hadi kufikia mwezi Juni, 2022 miradi 68 imeanza kutoa huduma ya maji kwa wananchi na miradi iliyobaki inatarajiwa kukamilishwa mwishoni mwezi huu na itanufaisha wananchi 1,036,071.

Alisema kwa mwaka huo RUWASA ilipokea Sh. bilioni 469.4 sawa na asilimia 94 ukilinganisha na kiasi cha Sh. bilioni 501.5 kilichoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji vijijini. Alifafanua kuwa kwa sasa, kati ya vijiji vyote nchini 12,319 ni vijiji 8,769 vinavyofikiwa na huduma ya uhakika ya majisafi na salama.

"Kwa mujibu wa tathmini iliyofanyika mwezi Aprili, 2022 upatikanaji wa huduma ya maji vijijini ulikuwa umefikia kiwango cha asilimia 74.5 ikiwa ni ongezeko la asilimia 9.7 ikilinganishwa na wastani wa 64.8 mwaka 2019. Kasi hii, ni nzuri na tukienda kwa kasi hii, tunatarajia kuvuka lengo la asilimia 85 ifikapo mwaka 2025, kama ilivyoelekezwa na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi," alisema.

**MWELEKEO 2022/23**

Katika mwaka huu wa fedha 2022/23, alisema RUWASA imepanga kutekeleza miradi 1,029, ambapo kati ya miradi hiyo 381 ni mipya na miradi 648 ile ambayo utekelezaji wake unaendelea kutoka mwaka wa fedha uliopita huku Sh. bilioni 387.7 zikitengwa kwa ajili hiyo.

Kwa upande wake, Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema Idara ya Habari Maelezo imeanza utaratibu wake wa taasisi za serikali kueleza mafanikio na mwelekeo wa mwaka wa fedha 2022/23.

Pia alisema wamesitisha taarifa za kila mwezi za msemaji huyo hadi utaratibu huo utakapomalizika.




Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mhandisi Clement Kivegalo, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, kuhusu mafanikio ya utendaji wa wakala huo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Watu 22,000 wafa kila mwaka sababu ya matumizi kuni na mkaa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, amesema kila mwaka wastani wa watu 22,000 hupoteza maisha kwa kuvuta moshi unaotokana na matumizi ya kuni na mkaa wakati wa maandalizi ya chakula nyumbani au katika taasisi zikiwamo shule.

Amesema kwa kuona ukubwa wa tatizo hilo, serikali imetenga zaidi ya Sh. bilioni 10 kwa ajili ya uwekezaji katika sekta ya nishati mbadala ikiwamo matumizi ya gesi asilia badala ya kuni na mkaa.

Makamba aliyabainisha hayo jana wakati akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Queen of Family inayomilikiwa na Kanisa la Katoliki Jimbo la Kahama wakati akifungua mradi wa gesi mbadala uliojengwa kwa gharama ya Sh.milioni 141.4 ili kuondokana na matumizi ya kuni na mkaa shuleni hapo.

Alisema matumizi ya gesi asilia ni njia mbadala kwa wananchi na utunzaji mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi husussani vijijini.

Kwa mantiki hiyo, Makamba alisema wananchi waishio vijijini watapewa kipaumbele ili kuondokana na matumizi ya kuni na mkaa ambayo kwa kiasi kikubwa yametajwa kuwa na madhara kwao.

Pia alisema serikali imetenga fedha hizo kwa ajili ya kujenga mifumo ya gesi asilia nchini ili kupunguza matumizi ya mkaa na kuni katika taasisi zote zikiwamo shule za msingi na sekondari zinazomilikiwa na serikali.

"Kila mwaka Watanzania 22,000 hupoteza maisha kwa kuvuta hewa yenye sumu ya kobonimonoksaidi inayozalishwa kwenye kuni na mkaa pindi wanapopika chakula au kutengeneza mkaa jambo ambalo serikali imechukua hatua ya kulitatua kwa kutenga Sh. bilioni 10," alisema.

Sambamba na hilo, alisema katika bajeti ya mwaka 2022/23 serikali kupitia Wizara ya Nishati, imejipanga kutoa elimu kwa wananchi kutumia gesi asilia katika kupika chakula na kuondokana na matumizi ya mkaa na kuni ambayo yana madhara katika afya zao kila siku.

Akitoa taarifa ya mradi huo kwa niaba ya Mkuu wa Shule hiyo, Mwalimu Hezekia Mafuru alisema ujenzi wa mradi huo ulianza mwaka jana kwa Sh. milioni 66.6 huku serikali ikiwasaidia Sh. milioni 47 hali ambayo inafanya gharama kufikia Sh. milioni 141.4 hadi kukamilika kwake.

Mafuru alisema shule hiyo ina wanafunzi 368 ili kuwapikia chakula walilazimika kutumia mkaa na kuni nyingi hali ambayo ilikuwa hatari kwao na wapishi. Lakini baada ya kujenga mradi huo, wameondokana na matumizi hayo na wanafunzi wao wana afya njema.

Vilevile, alisema uwapo wa mradi huo pia unatumika katika kujifunzia kwa wanafunzi kwa vitendo juu ya gesi asilia ili wanapohitimu elimu yao ya sekondari wakawe mabalozi wazuri katika utunzaji wa mazingira.

Mbunge wa Kahama Mjini, Jumanne Kishimba, alisema wanashukuru kanisa kwa kuwa mstari wa mbele katika kufanikisha kuwapo wa mradi huo na yeye atahakikisha anahamasisha wamiliki wa shule zingine kuiga mfano huo ili kuondokana na matumizi ya mkaa na kuni.

# Tanga kuanza huduma upasuaji uzazi pingamizi

**Na Mary Geofrey**

HOSPITALI ya Jiji la Tanga, inatarajia kuanza upasuaji wa uzazi pingamizi na kupokea wagonjwa wa rufani kuanzia Septemba, mwaka huu, baada ya kupokea vifaa tiba vya kisasa kutoka Bohari ya Dawa (MSD).

Akizungumza jana mkoani humo, Mganga Mkuu wa Wilaya ya Tanga Jiji (DMO), Dk. Charles Mkombe, alisema hospitali hiyo ni kati ya mpya vituo vya kutolea huduma za afya 67 vipya na vilivyofanyiwa ukarabati na serikali.

"Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, imelenga kuziwezesha hospitali hizo kupokea wagonjwa wa rufani na tayari tumepokea vifaa tiba vya kisasa vilivyotolewa na serikali kutoka MSD ambapo hivi karibuni tutaanza upasuaji," alisema.

Dk. Charles, alisema lengo la maboresho hayo katika sekta ya afya hususani huduma ya mama na mtoto ni kuimarisha sekta hiyo na kuchochea uchumi.

Aliongeza kuwa, hospitali hiyo inayohudumia wananchi 260,000 ilikuwa haifanyi upasuaji na kwa maelekezo ya Rais Samia Suluhu maandalizi yote yamekamilika ikiwamo watumishi wa kutosha, mazingira wezeshi yenye majengo 10 ya kisasa na vifaa tiba vya kisasa.

Naye Mteknolojia wa Mionzi wa hospitali hiyo, Mohamed Ally, alisema vifaa tiba na mashine zilizopokelewa kutoka MSD ni pamoja na vifaa vyote vya wodi ya kujifungua ikiwamo mashine ya Utra Sound yenye uwezo wa kupima moyo na kuchapa picha.

Alisema mashine hiyo inaweza kupima afya ya mtoto iwapo amezaliwa salama bila tatizo, mfumo wa damu wa mama, matarajio ya kujifungua, mtoto amefikisha muda gani akiwa tumboni na namna alivyokaa kabla ya kujifungua.




Mshauri Elekezi wa Mpango wa Uhamishaji watu na Makazi katika mradi wa Tembo Nickel kutoka kampuni ya RSK, Basil Shio (wa pili kushoto), akizungumza wakati wa kutangaza tarehe ya katazo la maendeleo ya ardhi katika eneo la mradi huo, wilayani Ngara, mkoani Kagera. Kushoto kwake ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Kanali Mathias Kahabi na Ofisa Tawala wa wilaya hiyo, Vedastus Tibaijuka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ulega ataka mapinduzi sekta ya mifugo, uvuvi

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amewataka watafiti katika sekta hiyo, kufanya utafiti utakaosaidia kuleta mapinduzi katika sekta hiyo nchini hususani katika kuimarisha uchumi wa buluu.

Ulega alitoa kauli hiyo alipofungua mkutano wa watafiti wa masuala ya uvuvi na viumbe maji uliofanyika mkoani Dar es Salaam.

Alisema ni lazima wanasayansi kuongoza mapambano kuhakikisha rasilimali za mazao ya baharini yananufaisha wananchi.

"Fursa ni kubwa katika sekta hii ya uvuvi, lakini bado hatujaitumia vizuri na naomba wataalamu mliangalie hilo. Bado tuna mgogoro na wavuvi ambao wanatumia zana haramu kwenye uvuvi ikiwamo 'ring net' pamoja na gesi, kwa hiyo inabidi mhakikishe mnatafiti vitu ambavyo vitasaidia wavuvi kunufaika na shughuli zao za uvuni na mkiendelea kuchelewa kufanya hivyo wao wataendelea kuharibu rasilimali zetu," alisema Ulega.

"Kutokana na harakati na mihangaiko ya kujitafutia riziki, wenzetu hawa huwa wanajikuta wanatafuta mbinu mbadala za kufanya shughuli zao zinawaletea manufaa, kwa hiyo inabidi ninyi wanasayansi muwe mbele zaidi yao kwa kujua vitu vinavyofaa kwenye sekta hiyo kulingana na mahitaji ya wakati husika, mara nyingi mnakuwa nyuma na ndiyo maana wakati mwingine wanatumia nyenzo au zana zisizo stahili na tutakuwa tunarudi nyuma."

Alisema tayari kwa upande wa serikali imejipanga kuweka nguvu kubwa kupitia bajeti kuu ya serikali pamoja na miradi mbalimbali kwa ajili ya kuendeleza sekta hiyo ya uvuvi na uchumi wa buluu.

"Uchumi wa buluu ndiko dunia inaelekea, kwa hiyo na sisi lazima tuwekeze nguvu kubwa huko kwa kuhakikisha tunainua uchumi wetu kupitia sekta hii," alisema Ulega.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), Dk. Ismael Kimirei, alisema lengo la mkutano huo ni kuhakikisha wanakuja na majibu ya kutatua changamoto zilizopo katika sekta hiyo pamoja na kuinua zaidi.

Alisema mkutano huo umejumuisha washiriki kutoka nchi mbalimbali ikiwamo Kenya, Uganda, Burundi na lengo ni kuhakikisha wanainua uchumi wa buluu jumuishi.

Ofisa Utafiti kutoka Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar (ZAFIRI), Ali Said Ali, alisema endapo wataalamu hao watafanya kazi kwa ushirikiano itakuwa rahisi kupatikana kwa majibu na changamoto zote zinazoikabili sekta hiyo.

# Huduma uunganishaji umeme zaboreshwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAZIRI wa Nishati, January Makamba amesema serikali imeboresha huduma za kuunganishiwa umeme kwa wananchi bila urasimu kama zamani.

Makamba alibainisha hayo jana mkoani Shinyanga, wakati akizungumza na viongozi wa Chama cha Mapinduzi (CCM), mkoani humo kabla ya kuanza ziara yake.

Alisema Shirika la Umeme Nchini (TANESCO), huduma zake kwa sasa zimeboreshwa na bado wanaendelea kuboresha zaidi ili kuhakikisha zinakuwa imara pamoja na kufungwa kwa wakati.

"Sasa hivi kuunganishiwa umeme hakuna urasimu tena kama zamani, ukiomba umeme kuunganishiwa ni siku saba tu na hakuna kutoa hata senti, zamani kupata umeme ilikuwa inachukua hadi miaka miwili au mpaka kujuana na mtu pale TANESCO," alisema Makamba.

Aidha, alisema Mkoa wa Shinyanga utaendelea kupata umeme wa uhakika baada ya mradi wa umeme wa jua megawati 150 unaotekelezwa wilayani Kishapu kukamilika.

Alisema umeme huo utaingizwa kwenye gridi ya taifa ili kumaliza tatizo la uhaba wa nishati hiyo mkoani humo.

Pia, anafahamu mkoa huo unahitaji umeme wa uhakika kutokana na shughuli zake za kiuchumi ukiwamo uchimbaji wa madini pamoja na viwanda vya uchakataji mazao mbalimbali.

Katika hatua nyingine alisema jitihada za kuboresha huduma ya upatikanaji wa umeme mkoani Shinyanga zinaendelea na hadi kufikia mwaka 2023 vijiji vyote mkoani humo vitawashiwa.

Awali, Katibu wa CCM mkoani Shinyanga, Donald Magesa, alisema wananchi wa mkoa huo wanalalamikia urasimu wa kuunganishiwa umeme.

Alisema inachukua muda mrefu mtu kupata umeme licha ya kulipia gharama zote. Mwaka mzima unapita akiwa anasubiri kufungiwa umeme na kwamba alilazimika kutumia nafasi yake ya ukatibu ndipo akapata.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, alisema mkoa huo hauna umeme wa uhakika jambo linalokwamisha shughuli za uwekezaji wa viwanda.

"Umeme hapa mkoani Shinyanga ni tatizo hautoshelezi, viwanda vingi havifanyikazi sababu hakuna umeme wa uhakika," alisema Mjema.

# Mnada wa wafugaji waonyesha fursa

**Na Frank Monyo**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), imeshiriki kikamilifu katika maonyesho na mnada wa mifugo, ambao ni wa kwanza kufanyika nchini, ukiwa na lengo la kuonesha mbegu mbalimbali za mifugo.

Mnada huo pia ulikuwa na lengo la kutoa fursa kwa wafugaji kujifunza ufugaji kibiashara kupata elimu na kubadilishana uzoefu. Maonyesho hayo yameratibiwa na Chama cha Wafugaji Mifugo Kibiashara Tanzania (TCCS).

Akizungumza jana wilayani Chalinze kunakofanyika mnada huo, Ofisa Mwandamizi wa TADB, Furaha Sichula, alisema hadi sasa TADB imeongeza tija katika sekta ya mifugo kwa kuwekeza zaidi ya Sh. bilioni 42 ambazo kati ya hizo, Sh. bilioni 14.2 zimekwenda kwenye sekta ndogo ya nyama ikiwamo ujenzi wa viwanda viwili vya kuchakata nyama.

"TADB pia imetoa Sh. bilioni 13.5 kwenye sekta ndogo ya maziwa ikiwamo viwanda vinne vya kusindika maziwa, Sh. bilioni 7.5 zimekwenda kwenye sekta ndogo ya kuku na 6.8 imeenda kwenye sekta ya uvuvi wa ufugaji wa samaki kwenye vizimba," alisema Sichula.

Aliongeza kuwa TADB inalenga kufikia Watanzania wengi zaidi katika sekta za mifugo, kilimo na uvuvi ili kuongeza uchumi wao na maendeleo ya sekta nzima.

Katika maonyesho hayo, viongozi mbalimbali walitembelea banda la TADB na kuishukuru kwa jinsi ambavyo inajitoa zaidi katika kuleta maendeleo ya sekta hizo adhimu katika uchumi wa nchi.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, aliishukuru TADB kwa kuwasaidia katika maeneo mengi na kuomba benki hiyo kutoa msaada zaidi katika kuwezesha mikopo ya sehemu ya malisho, ili kuepusha mifugo kuhamahama na kuhama kutoka kufuga kienyeji na kuanza kufuga kibiashara.

Mmoja wa mfugaji aliyeshiriki katika maonyesho hayo, Leng'idu Niwuyai, alisema TABD imekuwa na mchango mkubwa katika kuwasaidia wafugaji wadogo kufuga kisasa kupitia mikopo.

"Tumekuwa tukipata mikopo ambayo imetusaidia sana sisi wafugaji wadogo kufuga kisasa, hivyo kufanya kazi yetu hii iwe na faida. Tunaiomba TADB iwafikie wafugaji wengi zaidi ili kuongeza tija kwa sekta hii husasani kwa wafugaji wadogo," alisema.

## Wakulima sasa kupata pensheni

**Na Gideon Mwakanosya,**
TUNDURU

WAKULIMA wanaouza mazao yao kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani wanatarajia kuanza kupata pensheni ya uzeeni.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Usimamizi wa Mfumo wa Stakabadhi Ghalani Tanzania, Asangye Bangu, akizungumza juzi na vyama vya ushirika vya msingi vya Ligunga, Namatili na Mtetesi wilayani hapa, alisema serikali imedhamiria kuhusisha mfumo wa stakabadhi ghalani na pensheni kwa wakulima ili kumudu kuendesha maisha yao wanapokuwa wazee.

Alisema uwezo wa kufanya kazi kwa wakulima wakiwa vijana ni tofauti na wanapofikisha miaka 60, hivyo watakaokuwa wanauza kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani michango yao kidogo kidogo itafanyika kwenye mfumo ili kujiwekea akiba ya uzeeni.

"Nguvu zinapokuwa zimepungua, mashamba bado unayo, hivyo pensheni itawawezesha wakulima wazee kuendelea kupata fedha za kuwalipa vibarua watakaokuwa wanawafanyia kazi za kilimo," alisisitiza Bangu.

Hata hivyo amesema pensheni hiyo kwa wakulima itaunganishwa na mambo mengine muhimu kwa wazee kama bima za afya na mikopo.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, serikali iko katika hatua za awali za kuhakikisha kuwa suala la pensheni kwa wazee linafanikiwa.

Bangu alibainisha kuwa wataalamu watapita kwa wakulima ambao watapenda kujiunga kwenye mfumo huo ili kutoa elimu ya uelewa kabla ya kuanza utekelezaji wake.

Alisema licha ya kwamba pensheni kwa wakulima ni jambo geni, litakuwa msaada mkubwa kwa wakulima na kwamba litaongeza hamasa kwa vijana ambao bado wana nguvu lakini baada ya miaka kadhaa watafikia uzeeni.



Mkurugenzi wa Bodi ya Usimamizi wa Mfumo wa Stakabadhi Ghalani nchini, Asangye Bangu (kushoto), akizungumza na wanachama wa chama cha msingi cha ushirika Ligunga, wanaotumia mfumo wa stakabadhi ghalani katika kijiji cha Ligunga, wilayani Tunduru, jana. **PICHA: GIDEON MWAKANOSYA**

## Serikali kuongeza uzalishaji miwa Kilombero

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

SERIKALI imedhamiria kuongeza uzalishaji wa miwa nchini kwa kuwekeza kwenye ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya wakulima wadogo na kuhimiza matumizi ya mbegu bora.

Mkakati huo wa serikali ulitangazwa na Waziri wa Kilimo, Hussen Bashe, mjini hapo juzi wakati akifungua mkutano wa 10 wa wadau wa sekta ndogo ya sukari nchini, uliohudhuriwa pia na Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji.

Aidha, Waziri Bashe aliagiza Bodi ya Sukari Tanzania kushirikiana na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kuainisha maeneo ya mashamba na kufanya vipimo na kuwekeza kwenye ujenzi wa miundombinu kwa kuwa asilimia kubwa ya wakulima wa miwa wanategemea mvua.

Bashe alisema ili teknolojia ya umwagiliaji ifike katika mashamba ya miwa ni lazima Bodi ya Sukari ifanye kazi na tume ya taifa ya umwagiliaji kwa kuyabaini mashamba ya wakulima, ili kujua ni teknolojia gani ya umwagiliaji itatumika.

Kwa mujibu wa Bashe, wakulima wadogo wa miwa wana mchango mkubwa kwenye uzalishaji wa miwa na kwamba ni lazima kuboresha miundombinu ya kilimo ili kichangie pato la taifa.

Waziri huyo alitolea mfano uwekezaji wa miundombinu utakaofanywa katika bonde la Kilombero lenye wakulima wengi wa zao hilo kwamba litakuwa la kuigwa katika uzalishaji wa zao hilo.

Waziri Bashe pia aligiza Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kuhakikisha inafanya utafiti na kuanzisha vitalu vya mbegu bora ya miwa itakayokuwa na uzalishaji mkubwa ili ilitumiwe na wakulima.

Naye Waziri Kijaji aliwahimiza wadau wa sekta ndogo ya miwa kuwa na maandalizi katika kukabiliana na ushindani wa soko ndani na nje ya Afrika.

Alisema hakuna haja ya kuingiwa na hofu katika ulimwengu wa soko la ushindani kilichokuwa muhimu ni kuendesha kilimo chenye tija kwa kuongeza uzalishaji licha ya serikali kuruhusu uwekezaji wa kilimo hicho.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Sukari Tanzania (SBT), Prof. Kenneth Bengesi, alisema upungufu wa sukari unatokana na tija ndogo katika uzalishaji wa miwa hasa kwa wakulima wadogo kwa kuwa aina ya mbegu wanazotumia hazina tija wala kukabilina na changamoto ya ukame.

Mmoja wa wakulima wa zao hilo katika bonde la Kilombero, Bakari Mkangamo, aliishukuru serikali kwa kuwasaidia wakulima wadogo wa miwa ili waondokane na kilimo cha mazoea kinachotegemea mvua na badala yake kushiriki katika kilimo cha umwagiliaji na matumizi ya mbegu bora .

# Watanzania wahamasishwa kuchangamkia fursa elimu

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Elimu Nje ya Nchi, Global Education Link (GEL), imewataka Watanzania kuchangamkia fursa ya ufadhili wa Jumuiya ya Madola kwa ajili ya kusoma nchini Uingereza zinazotarajiwa kufunguliwa kuanzia wiki ijayo.

Kila mwaka Uingereza inatoa nafasi 35 kwa Watanzania kwenda kusoma bure nchini humo, lakini ni wastani wa watu 10 hadi 15 wamekuwa wakifanikiwa na wengine hukosa kwa kushindwa kujaza vizuri maombi yao.

Mkurugenzi Mtendaji wa GEL, Abdulmalik Mollel, alisema hayo jana kwenye maonyesho ya vyuo vikuu yanayoendelea kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam.

Maonyesho hayo yanahudhuriwa na vyuo mbalimbali vya ndani vikiwamo 10 vya nje ya nchi vilivyokuja kwa mwavuli wa GEL.

Baadhi ya vyuo hivyo vinatoka Iran, India, Georgia, Cyprus, Uturuki, Marekani, Uingereza, Mauritius, Dubai, Poland, Australia, Canada na Malaysia.

Alisema GEL imeangalia kozi zenye uhitaji zaidi kama zile za afya na huduma ambazo Watanzania wanazihitaji na kualika vyuo hivyo kwa ajili ya udahili kwa wale watakaohitaji kusoma kwenye nchi hizo.

Mollel alisema Watanzania wengi wanashindwa kupata nafasi hizo kutokana na kukosa uwezo wa kujaza maombi yao, na kwamba wakifika kwenye maonyesho hayo wataelimishwa.

Alisema ili kupata ufadhili huo mhusika anapaswa kufanya mtihani wa International English Language Testing System (IELTS), unaopima ufahamu wao kwa lugha ya Kingereza, lakini wengi wamekuwa wakishindwa kutokana na kutokutimiza vigezo katika mchakato wa maombi yao.

"Watanzania wengi wamekuwa wakiwasilisha maombi kusoma Uingereza kwa ngazi mbalimbali, lakini wanashindwa sasa British Council wako kwenye mabanda ya Global Education Link kwa ajili ya kuwaelimisha Watanzania namna ya kujaza vizuri maombi yao na kupata ufadhili," alibainisha Mollel.

Akizungumza kwenye maonyesho hayo jana, ofisa kutoka British Council, Tamara Bwire, alisema wamehudhuria maonyesho hayo ili kutangaza mitihani ya IELTS ambayo wamekuwa wakiifanyisha kila mwezi kwa watanzania wanaotaka kwenda Uingereza na nchi mbalimbali duniani.

British Council, alisema inaratibu ufadhili kwa wanaotaka kwenda Uingereza kuongeza elimu yao kuanzia ngazi ya shahada ya uzamili katika vyuo vya nchini humo.

Alisema moja ya vigezo vya watu kupata ufadhili huo ni kuwa raia wa nchi inayotoka Jumuiya ya Madola kama Tanzania na awe na ufaulu wa kuanzia daraja la pili la juu wa 'Upper Second Class'.

Alitaja kigezo kingine cha mwombaji kupata ufadhili huo awe amepata udahili kwa moja ya vyuo vya Uingereza na kwamba kuanzia wiki ijayo ufadhili huo utafunguliwa.




Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa (kushoto), akizungumza katika uzinduzi wa Programu ya Mwalimu Spesho, wilayani Karagwe, mkoani Kagera juzi. Wengine ni Mkuu wa Idara ya Biashara za Serikali ya Benki ya NMB, Vicky Bishubo (kulia), Meneja wa NMB Kanda ya Ziwa, Baraka Ladslaus (wa pili kulia) na Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi, Aikansia Muro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafanyabiashara 13,000 wasajiliwa kudhibiti ubora

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAZALISHAJI na wafanyabiashara wa mbegu wapatao 13,873, wamesajiliwa na Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu (TOSCI).

Lengo la usajili huo ni kudhibiti ubora ikiwa ni mkakati wa kuhakikisha wakulima nchini wanapata mbegu zenye ubora na kuleta tija katika kilimo.

Mkurugenzi Mkuu wa TOSCI, Patrick Ngwediagi, alisema juzi kuwa lengo la kuwasajili ni kuondoa malalamiko yaliyokuwa yakitolewa na wakulima kuuziwa mbegu zisizo na ubora hatua iliyosababisha wakulima kupata hasara.

Ngwediagi alisema kwa upande wa wafanyabiashara waliosajiliwa mpaka sasa wamefikia 6,936, wauzaji wa mbegu ni 5,559, wakulima wanaojishughulisha na 964 pamoja na kampuni 413.

Alisema licha ya manufaa kwa wakulima kupata mbegu bora, pia wazalishaji hao kutoka sehemu mbalimbali nchini watakuwa na uhakika wa kuuza katika soko la ndani na nje ya nchi.

Mkurugenzi huyo alifafanua kuwa uhakika wa soko la nje unatokana na TOSCI kujiunga na skimu ya mbegu ya shirika la kimataifa linatambua ubora wa mbegu katika nchi mbalimbali (OECD).

Alisema uhakika mwingine kwa wazalishaji kuuza mbegu zao kwenye nchi yoyote inatokana na TOSCI pia kuwa mwanachama wa Taasisi ya Kimataifa ya Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea (UPOV) huku ikiwa na Hati ya Ithibati ya Kimataifa (ISTA).

"Kwa sasa TOSCI inatambulika kwenye viwango vya kimataifa kutokana na kudhibiti ubora wa mbegu hivyo wazalishaji wetu wanaweza kuuza kwenye nchi yoyote," alisema.

Alisema mafanikio ya kudhibiti ubora wa mbegu kitaifa na kimataifa inatokana na ongezeko la mbegu zilizothibishwa ubora katika kipindi cha mwaka 2014 /15 -2019/20.

Mkurugenzi Mkuu huyo alisema katika kipindi hicho, TOSCI ilizifanyia majaribio ya aina mpya za mbegu, kukagua mashamba, kufanya majaribio ya sampuli na kufanya vipimo kwenye mbegu zilizozalishwa, ili kuhakiki ubora wake.

Kuhusu mbegu feki na dhaifu zilizokuwa zikiuzwa kwa wakulima nchini na kuwasababishia hasara, alisema sasa suala hilo limedhibitiwa kwa asilimia kubwa kutokana na kuongeza kasi ya matumizi ya lebo zake zenye ubora katika mbegu zinanazozalishwa.

Naye Waziri wa Kilimo, Hussen Bashe, alisema mkakati uliopo sasa ni kuhakikisha taasisi zote zenye uwezo wa kuzalisha mbegu bora zinafanya hivyo kwa usimamizi wa TOSCI, ili kuhakikisha wakulima wanapata mbegu zinazokidhi viwango na wale wote watakaouza mbegu feki kwa wakulima hatua kali dhidi yao zitachukuliwa.

# Wafugaji watakiwa kuzalisha kwa tija

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

MWENYEKITI wa Chama cha Wafugaji wa Kibiashara Tanzania (TCCS), Naweed Mulla, amewataka wafugaji kubadilika katika ufugaji ili kupata tija na kuuza mifugo yao ndani na nje ya nchi.

Mulla aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuhitimisha maonyesho ya mifugo ya siku tatu yofanyika Ubena, Chalinze ambayo yaliandaliwa na chama hicho kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB).

Mwenyekiti huyo alisema lengo la maonyesho hayo ambayo yaliambatana na elimu kwa washiriki, yalilenga kuelimisha namna ya kufuga kibiashara na kuwawezesha wafugaji kunufaika na mifugo yao.

Alisema katika maonyesho hayo elimu ya namna bora ya kupata malisho, dawa za mifugo na kufuga kisasa ilitolewa ambapo wataalamu mbalimbali walishiriki na kufundisha kuhusiana na ufugaji wa kisasa ambao utakuwa mkombozi katika ufugaji na kumfanya anufaike na mifugo yake.

"Mtu ambaye anaelewa mifugo atalipa kinachostahili. Hii imejidhihirisha kwenye maonyesho haya kupitia minada ya mifugo ambayo imefanyika na kuwezesha ng'ombe mmoja kuuzwa kwa Sh. milioni 13 lakini yupo pia aliyekuwa na bei ya juu zaidi ya Sh. milioni 40," alisema.

Mulla ambaye ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Highland Estate, alisema maonyesho hayo yataendelea kufanyika kila mwaka kwa namna watakavyokuwa wanajipanga katika chama chao kuwafikia wafugaji na kutoa elimu ya ufugaji wa kibiashara ambao pia utaondoa migogoro na kufuata taratibu.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Mkoa wa Pwani, Ngobere Rashidi, alisema maonyesho hayo yamefanyika kwa muda mwafaka kwa kuwa yamesaidia kufikisha elimu ya kufuga kibiashara na kuwaondoa wafugaji kwenye ufugaji wa asili.


Ngobere pia alisema kupitia maonyesho hayo, wafugaji wamenufaika na elimu ya namna ya kuandaa malisho ya mifugo yao njia ambayo itawaondolea tabia ya kuhamahama na kupunguza migogoro ya ardhi.

Baadhi ya washiriki wa maonyesho hayo wakiwamo wasambazaji wa dawa za mifugo wa kampuni ya Tansoko Agrovet, walikishukuru chama hicho kwa kuwashirikisha na kuwakutanisha na wafugaji na kuwapatia elimu ya dawa wanazozisambaza.



Ukurasa 13

**Uwanja wadaiwa si sawia kwa wapinzani**



Ukurasa 14

Ndivyo historia uongozi wa kabila moja Kenya inavyoelekea ukingoni



Ukurasa 12

**Rais Samia alivyo alama na tunu ya uwezo wa wanawake kuongoza**


# siasa

JUMATANO JULAI 20, 2022

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU


# Tanzania inapomkumbuka Mkapa

## • Ni wakati wa kurejea kumbukumbu nyingi za mageuzi aliyoifanyia nchi

**Na Gaudensia Mngumi**

MWEZI Julai unaacha alama kwenye historia ya uongozi wa Tanzania, ndicho kipindi japo kwa nyakati tofauti viongozi wa serikali ya awamu ya tatu, Benjamin Mkapa na Makamu aliyeanza naye kazi, Dk. Omar Ali Juma, walifariki dunia.

Julai 4, mwaka 2001, Dk. Omar, alifariki dunia na kumuacha Rais Mkapa katika kitendawili, maana walitumika pamoja kwa wastani wa miaka sita ya awamu ya tatu, wakiwa na mengi ya kutekeleza pamoja.

Mkapa, maarufu kwa jina la Ben, aliendelea kuongoza akiwa na makamu mpya, Dk. Ali Mohammed Shein, hadi alipomkabidhi kijiti Rais Jakaya Kikwete -JK, Ben akibaki mstaafu na mzee wa heshima anayeshauri serikali, chama pia akiwa na majukumu mengine ya kimataifa.

Baada ya miaka 20 ya kifo cha Dk. Omar, Julai 24 Mkapa alifariki dunia, huku nyayo zake za kihistoria zikiacha mengi ya kiutendaji yasiyofutika kwa Watanzania, kuanzia utumishi wake kwenye Baraza la Mawaziri, akiwa na umahiri kwenye diplomasia, hadi ukuu wa nchi.

Siku nne zijazo, kwa maana ya Jumapili ijayo itatimu miaka miwili ya kifo chake shujaa huyo, mzaliwa wa Masasi mkoani Mtwara na nahodha wa mageuzi ya kiuchumi nchini, alikotumikia kwa kina jukumu la ubinafsishaji.

Katika awamu yake ya uongozi, Ben alitekeleza kwa kuunda nyenzo nyingi za sura ya nchi inakoelekea, kuendeleza yaliyoasisiwa na mtangulizi wake, Ali Hassan Mwinyi- 'Mzee wa Ruksa'.

Kisiasa, kupitia uchaguzi mkuu alikuwa wa kwanza kutoka chama tawala CCM, kuchuana na makali ya ushindani kutoka kwa wagombea wa upinzani na hasa Augustino Mrema,




Hayati Benjamin Mkapa. **PICHA: MTANDAO**

aliyevaa kofia ya NCCR-Mageuzi akiungana na baadhi ya vyama vingine, Mkapa akiibuka na zaidi ya asilimia 60 ya kura.

Leo Watanzania wanapoadhimisha miaka 30 ya vyama vingi, hawatausahau mchango wa Mkapa katika kufanikisha siasa za vyama vingi.

Ni nguvu za Mkapa katika kuendeleza demokrasia akaanzisha utaratibu wa kuvipa ruzuku vyama hivyo ili viwe na mtaji wa kisiasa na nguvu ya kuonekana hadharani kwa vile vingi vilikuwa vichanga bila hazina wala akiba ya kupangisha ofisi.

Kadhalika wanaotazama juhudi za kubadilisha mifumo ya uchumi na kuipa sekta binafsi rungu la kuendeleza uchumi hawatamsahau Mkapa.

Kwa upande wa taasisi za umma, anakumbukwa kwa namna ya pekee alivyoisimamia mageuzi yake, chini ya Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC), akihimiza serikali zaidi itabaki na majukumu ya kusimamia sera, sheria na kujenga mazingira wezesha ya uwekezaji wa sekta binafsi.

Ndiye aliyeliasisi jukwaa la Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF) kama sauti ya sekta binafsi na katika sekta zote za uchumi, vikiwemo vyama vya wafanyabiashara akaikabidhi jukumu la injini ya uchumi.

Falsafa yake mara zote alihimiza kutokukubaliana na hali duni kwenye huduma za fedha, huku ambako kulishuhudiwa mageuzi makubwa ambayo yanaendelea kuchukua sura tofauti hadi sasa kulingana na matakwa ya wakati.

Kwa upande wa hitaji muhimu la nishati, Ben alieleza namna alivyotamani kuwapo Tanzania isiyo na giza na katika hatua ya utekelezaji wake, kuna ushuhuda wa mradi wa umeme wa gesi asilia wa Songo Songo, ambao si sisimulizi mpya kwa Watanzania.

Sura ya utekelezaji wake ilichukua nafasi Julai 2008, pale gesi ya Songo Songo mkoani Mtwara ilipofika katika kituo kikuu cha umeme Ubungo Dar es Salaam na ukawa mwanzo wa kusambazwa umeme wa gesi kitaifa.

Wakati anaondoka madarakani akaacha kiwango cha uzalishaji umeme kitaifa kikiwa wastani wa megawati 447, kijiti cha hatua hiyo kwa awamu zilizofuata kimeendelezwa na sasa uzalishaji ni takribani megawati 1,700.

Hizo zinapatikana kutoka vyanzo mbalimbali ama alivyoanzisha, kuendeleza na baadhi vya ndoto zake zikijumuisha: Mitambo ya Kinyerezi 1 na 2, pia kiwanda cha kuchakata gesi asili ya mitungi

Mkuu huyo wan chi ana alama karibu kwenye kila sekta, mathalani, katika eneo alilolipenda sana, hakuficha kukereka sana kuona Tanzania haina wasomi wengi wa elimu ya juu.Ni hatua iliyoenda sambamba na mchakamchaka wa ujenzi na upanuzi wa shule za sekondari za kata.

Ili kuweka mazingira wezeshi ya kuwasaidia wasomi wa elimu ya juu akaunda chombo mahsusi, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) iliyoanza kazi mwaka 2005, ambayo matunda yake yanashuhudiwa hivi sasa.

Itikadi aliyoiunda ni haja ya kuwepo Watanzania wengi wasomi na idadi yao iwe kubwa kwenye kujiajiri na kufanyakazi kwenye sekta binafsi ambayo kwake ilikuwa injini ya uchumi.

Wiki hii Watanzania na dunia wanapomkumbuka rais wao wa awamu ya tatu, Benjamin William Mkapa, kuna mengi yanayobaki alama ya nyayo za kazi zake.

# Rais Samia alivyo alama, tunu ya uwezo wa wanawake kuongoza



Rais Samia anatazamwa kama tunu ya uongozi shujaa wa wanawake. **PICHA: MAKTABA**

**Na Victoria Mwanziva**

BABA wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, aliwahi kusema "inawezekana tatizo la paka kwa panya ingekuwa kwa paka kufungwa kengele shingoni lakini tabu ni kumpata wa kufanya kazi hiyo. Na panya watakua wajinga wakidhani paka watajifunga au kufungana kengele".

Kauli hii ya Baba wa Taifa kwangu naichukulia katika nyanja ya uongozi kwa wanawake, kwani naamini wanawake hawawezi kuinuka na kuifikia azma ya kujenga usawa katika uwanja wa uongozi kwenye jamii yao kwa kusubiria fadhila au kuwezeshwa na wanaume.

Wanawake tunatakiwa kusimama, kuinuana, kufundishana na kujengana kupigania usawa huo na kuinuana.

Awamu hii ya sita wanawake wanaye mkombozi halisi ambaye kwa sasa amemfunga paka kengele na ndiyo wakati wanawake wanatakiwa kuzidi kuonyesha uwezo wao wa uongozi katika nafasi zao.

Tangu mataifa ya Tanganyika na Zanzibar yalipoungana mwaka 1964 na kuzaliwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tumepita katika vipindi mbalimbali vya uongozi kuanzia awamu ya kwanza ya Mwalimu Nyerere, hadi sasa awamu ya sita ya Rais Samia Suluhu Hassan na katika awamu zote tumeshuhudia ushiriki wa wanawake katika nyanja mbalimbali za uongozi na tunashuhudia katika kila zama za uongozi, idadi ya wanawake katika uongozi inaongezeka.

Aidha, watoto wa kike wengi wanahamasika kushiriki katika shughuli mbalimbali za kujifunza na kukua katika sekta hiyo ya uongozi.

> Wanawake mmezaliwa na uwezo sawa na wanaume, mkiwa na uwezo wa kutimiza mambo makubwa, lakini jamii na baadhi ya watu wamewafanya muamini kuwa hamuwezi, kataeni dhana hiyo kwa kuonyesha kuwa mna uwezo.

Katika historia ya taifa letu tuna wanawake wengi na mashuhuri walioongoza mapambano mbalimbali ya kulikomboa taifa kuanzia kudai uhuru, na baadaye wakaendelea na harakati za kuikomboa jamii kutoka gizani na kuonyesha mwanga wa wanawake kwa kutambua mchango wao mkubwa katika kuonyesha na kudhihirisha uwezo wa uongozi ndani ya mwanamke katika taifa.

Bibi Titi Mohammed, Balozi Getrude Mongela, Balozi Dk. Asha Rose Migiro, Balozi Amina Salum Ali, Spika mstaafu Anne Makinda na wa sasa Dk. Tulia Ackson, Waziri Ummy Mwalimu, Angela Kairuki, Mabalozi Batilda Buriani, Hoyce Temu, Waziri Liberata Mulamula na Katibu Mkuu Kiongozi Zanzibar Zena Ahmed Said.

Hao ni miongoni mwa wengi ambao michango yao kwa maendeleo ya taifa hili ni alama isiyosahaulika na inawapa ari kubwa vijana wanawake wanaochipukia katika uwanja wa uongozi kutamani kufanya kama wao.

Ni ukweli usiofichika kuwa, wanawake wana uwezo mkubwa wa uongozi sawa na wanaume mkubwa duniani na changamoto kubwa miaka ya nyuma iliyowakumba kinamama katika nyanja za uongozi, ni kukatishwa tamaa na kushushwa chini na jamii zinazowazunguka, ikiaminika wanawake hawastahili kushika nafasi kubwa za uongozi, kwani jukumu lao la msingi ni kulea familia na kufanya kazi za nyumbani.

Dhana hii ilisababisha watoto wa kike kutokupelekwa shule, kwani jamii iliona hakuna haja ya kumsomesha binti ilhali hawezi kuwa na nafasi yoyote ya uongozi.

Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, aliwaasa wanawake na kuwasihi kukataa dhana ya kuambiwa kuwa hawana uwezo, ilhali wana uwezo mkubwa, akisema;

"Wanawake mmezaliwa na uwezo sawa na wanaume, mkiwa na uwezo wa kutimiza mambo makubwa, lakini jamii na baadhi ya watu wamewafanya muamini kuwa hamuwezi, kataeni dhana hiyo kwa kuonyesha kuwa mna uwezo".

Sasa tunashuhudia mapinduzi makubwa ya kiuongozi kutoka kwa kiongozi shupavu Rais Samia anavyoonyesha kwa vitendo na kuwashuhudia Watanzania na Afrika kwa ujumla kuwa yeye ni alama halisi ya uwezo wa uongozi uliopo ndani ya mwanamke.

Katika hotuba yake ya kwanza baada ya kuapishwa kuliongoza taifa aliwaaminisha Watanzania kuwa ana uwezo mkubwa wa uongozi na kuwaahidi halitaharibika jambo.

Aliikataa dhana ya wanawake kuonekana hawana uwezo wa uongozi na anaishi katika maneno ya Mwalimu Nyerere, mnamo Machi 22, mwaka jana katika Uwanja wa Jamhuri Dodoma, alisema "Naomba niseme kidogo, kwa wale wenye mashaka na mimi kwamba mwanamke huyu ataweza kuwa Rais wa Tanzania, nataka niwaambie kuwa aliyesimama hapa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye maumbile yake ni mwanamke".

Rais Samia amekuwa ni chachu ya kuwainua wanawake na kuona karama za uongozi zilizopo ndani yao, pia uwezo wao mkubwa katika nafasi za uongozi, katika hotuba yake Rais Samia alipokua anazungumza na wanawake Siku ya Demokrasia Duniani jijini Dar es Salaam, Septemba 15, 2021.

Alionyesha ni kwa jinsi gani anatamani kuona wanawake wanaendelea kuonyesha uwezo wao wa uongozi na kusaidiana ili kuifikia azma ya kweli ya 50/50 katika nyanja zote za kiongozi kwa kutatua changamoto ndogondogo zinazowakabili wanawake kwa kusema.

"Mpaka leo tunazungumzia wanawake wajasiriamali, wanawake wafanyabiashara wakubwa, lakini wanawake makondakta wako wengi nchini, ingawa bado kuna changamoto ndogondogo ambazo tunatakiwa kuzifanyia kazi ili waweze kufanya kazi zao".

Uongozi wa Rais Samia umetudhihirishia uwezo mkubwa walio nao wanaweka katika uongozi pengine kuliko hata baadhi ya wanaume waliowahi kupata nafasi za uongozi ngazi za juu katika taifa letu, tunashuhudia uongozi wa uwazi uliosheheni demokrasia na mapinduzi ya kimaendeleo.

Ndani ya Rais Samia tunashuhudia dhana halisi ya kiongozi anayejali maisha ya wananchi wake kwa asilimia 100 katika kupanga mikakati ya maendeleo kwa ajili ya taifa, tunaona utu na kama Watanzania tunavyomuita Mama basi anadhihirisha huruma ya Mama kweli kwa watoto wake Watanzania.

Wanawake wasipoinuka sasa na kudhihirisha vipaji vyao vya uongozi watakuwa wanamgharimu na kumkatisha tamaa Rais Samia ambaye kwa sasa amemfunga paka kengele.

Ndani ya CCM na jumuiya zake, sasa ni kipindi cha uchaguzi ambapo viongozi wanaochaguliwa watatumikia nafasi hizo kwa miaka mitano ijayo ni wakati sasa kwa wanawake kuinuka na kudhihirisha kweli Rais Samia amewainua na kuwaheshimisha katika uwanja wa uongozi kwa kujitokeza kwa wingi kuchukua fomu kugombea nafasi mbalimbali zilizoainishwa.

Kwa kufanya hivi tutakua tumefuta dhana ya mwanamke akiwezeshwa anaweza na kuwaambia watu duniani kuwa wanawake ni jeshi kubwa na uwezo wa uongozi wanao na sio kuwezeshwa pekee kunakowafanya waweze.

Wito wangu kwa wanawake na mabinti wote wanaochipukia katika uongozi ni kuziishi ndoto na maono yao waliyoyabeba kuhusu uongozi kwa kutimiza majukumu yao kadri inavyoelekezwa katika nafasi zao za uongozi na wanapopata nafasi kuonyesha ubunifu wa ziada na kamwe wasiruhusu kukatishwa tamaa na watu wasio na nia njema katika kuleta usawa katika jamii yetu.

Tuonyeshe uthubutu na tusaidiane na kuinuana pale tunapoona mwenzetu anaanguka tumuinue hii itawadhihirishia watu kuwa wanawake ni wamoja na wanaweza kufanya mambo makubwa kwa umoja wao na kuleta matokeo chanya katika taifa letu.

***Mwandishi ni Katibu Idara ya Uhamasishaji na Chipukizi UVCCM Taifa.***

# Miongo 3 vyama vingi uwanja wadaiwa si sawia kwa wapinzani

## • Mazingira magumu kiuchaguzi kila mwaka

Na Sabato Kasika

JULAI mosi mwaka huu, Tanzania imetimiza miaka 30 tangu kurejeshwa kwa mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa, ambao ulifungua mlango wa uchaguzi mkuu wa kwanza wa mfumo huo Novemba 1995.

Hayati Benjamin Mkapa ndiye alikuwa Rais kwanza kuchaguliwa ndani ya mfumo huo uliohusisha vyama kadhaa vya upinzani vilivyoshiriki, kikiwamo NCCR-Mageuzi ambacho wakati huo kilikuwa tishio wa CCM.

Mgombea urais kwa tiketi ya NCCR-Mageuzi alikuwa Augustino Mrema, ambaye kwa kiasi kikubwa alimtikisa Mkapa na kukifanya chama chake kupata wabunge 19 wa kuchaguliwa katika majimbo mbalimbali nchini.

Nguvu ya chama hicho ilimfanya Baba wa Taifa hayati Mwalimu Nyerere asimame imara kumpigia debe Mkapa baada ya kuona hali inaweza kubadilika na kuingia chama cha upinzani madarakani.

Ijumaa iliyopita, Kituo cha ITV kiliendesha kipindi cha Kipima Joto, mada ikiwa ni miaka 30 ya mfumo wa demokrasia ya vyama vingi Tanzania, Je, umefikia malengo ya kuasisiwa kwake'?

Washiriki katika kipindi walikuwa ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya, Abdul Kambaya na Kimishna Msaidizi Mwandamizi mstaafu wa Jeshi la Polisi ASP Jamal Rwambow.

### MALENGO BADO

Mwenyekiti wa CEGODETA ambaye pia ni kada wa CCM, Thomas Ngawaiya, anasema, hadi sasa miaka 30 tangu kurejeshwa kwa mfumo wa demokrasia ya vyama vingi, malengo ya kuasisiwa kwake hayajafikiwa.

"Kwa hakika kwa miaka hii 30 ya vyama vingi, tukisema tumefikia malengo si sahihi, hatujafikia malengo, tumepotea kabisa, kuna mambo madogo madogo yanayoendelea lakini sivyo tulivyoanza," anasema Ngawaiya.

Mwanasiasa huyo anasema malengo ya chama chochote cha siasa kiwe tawala au upinzani, ni kushika dola, na kwamba tangu wakati huo hadi sasa, hakuna chama cha upinzani ambacho kimeshika dola.

"Leo ni miaka 30 dola linashikiliwa na CCM. Maana ya kuanzisha vyama vya upinzani ilikuwa ni ushindani wa kisiasa ili kupata cheche yaani moto uwake kwa maana ya demokrasia ya kweli na maendeleo ya haraka," anasema.

Anakumbusha kuwa kabla ya mfumo huo kurejeshwa, hayati Jaji Francis Nyalali, alizunguka nchi nzima kutafuta maoni ya Watanzania kama wanataka mfumo huo, na kwamba asilimia 80 waliukataa, asilimia 20 wakaukubali.

"Busara ya Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere ilitumika kuruhusu asilimia 20 iheshimiwe, ndipo uchaguzi wa kwanza ukafanyika mwaka 1995 huku ukigubikwa na kasoro kadhaa zikiwamo za madai ya udanganyifu," anasema.

Mwenyekiti huyo anasema miaka yote, hakuna uwanja ulio sawa katika uchaguzi, na kwamba unaendeshwa kwa kuegemea upande mmoja na kuvifanya vyama vingine vikibaki kusindikiza badala ya kushika dola.

Hata hivyo, anasema kuna dalili njema za kushamiri kwa siasa, kwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan, ameonyesha nia hiyo ya kuweka sawa, kwa sheria kuheshimika pande zote mbili za chama tawala na upinzani, hasa kwenye suala la kufanya mikutano ya hadhara na maandamano.

"Rais ana nia njema ya kuturudisha kule tulikoanzia, mwaka 1992 ambapo siasa zilishamiri vizuri bila misuguano, lakini miaka ya hivi karibuni mambo yakaenda kinyume," anasema Ngawaiya.



Jamal Rwambow



Abdul Kambaya

> Katika mazingira hayo na ukiukwaji wa demokrasia ndani ya vyama hivyo, havitakuwa imara, vitaendelea kubaki kama vilivyo kama hakuna hatua za makusudi za kuvifanya vipige hatua kwenda mbele.



Thomas Ngawaiya

### NI HATUA KIDOGO

Abdul Kambaya, anaposhika kipaza sauti, anasema, kwa muktadha wa kuwapa Watanzania elimu ya uraia kuna hatua kidogo zimepigwa kwa miaka 30 ya mfumo wa demokrasia ya vyama vingi, kwa kuwa wananchi wanaelewa vizuri mfumo huo.

"Katika masuala ya uelewa wa demokrasia, Watanzania wamekuwa na uelewa mkubwa, ukisema utafiti kama wa Jaji Nyalali urudiwe leo idadi ya wanaotaka mfumo wa vyama vingi itakuwa kubwa," anasema Kambaya.

Anaongeza kuwa vyama vya upinzani vimefikia malengo ya kuelimisha Watanzania kujua lengo la kuanzishwa kwake na vimechangia kupatikana kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar.

Mwanasiasa huyo anasema, upinzani umefanikiwa katika mazingira magumu ya kiuchaguzi ambayo yamekuwa yakijitokeza kila mwaka wa uchaguzi na kwamba wanasiasa wanayajua mazingira anayosema.

Anasema, hatua hiyo ya kuelimisha Watanzania kuhusu vyama vya upinzani ni ya kujivunia, kwa madai kwamba imefikiwa katika mazingira magumu ambayo wanasiasa wangeweza kukata tamaa.

"Kinachotakiwa ni kumalizia tatizo la kiuchaguzi kwa kuwapo katiba mpya na tume huru ya uchaguzi ambayo itaendesha shughuli zake kwa uwazi na ukweli kwa kuruhusu Watanzania kuchagua watu wanaowataka.

Anasema, dalili za kufikia huko zimeanza kuonekana, ambapo anatamani zifikie matarajio ya Watanzania walio wengi ambayo ni kuchagua wagombea ambao wao wenyewe wanawataka.

### HAKUNA DEMOKRASIA

Kamanda Jamal Rwambow anasema kinachoshuhudiwa ndani ya miaka hiyo 30, ni kuwapo kwa ukiukwaji wa demokrasia ndani ya vyama vya upinzani hali ambayo inaweza kuwa ngumu kuvifanya vishike dola.

"Vyama vinaanzishwa vikiwa na katiba, ambayo viongozi wake wanaapa kuilinda na kuifuata, lakini utakuta vyama vingine wanachama wakijaribu kuhoji mambo yanayokwenda kinyume, wanafukuzwa," anasema Rwambow.

Anasema, waliodhani kupitia upinzani wanaweza kufikia malengo ya kuinua uchumi, wamekutana na migogoro, na kwamba hadi sasa kuna migogoro, ambayo inasababishwa na ukiukwaji mkubwa wa demokrasia ndani ya vyama.

"Kuna jambo ambalo watu hawajui, ni lengo la kuanzishwa kwa vyama hivyo, ambalo ni kuvipa nafasi kukuza uchumi wa taifa letu, ambapo utararibu uliwekwa viwe na muonekano wa kitaifa, si sura ya kibaguzi," anasema.

Anasema, wanasiasa walikubali masharti na kuanzisha vyama vya siasa bila kuwa na uchumi imara, na kwamba chama bila kuwa na uchumi ni tatizo, na kwamba vimebaki kutegemea fadhila, ruzuku na misaada.

"Katika mazingira hayo na ukiukwaji wa demokrasia ndani ya vyama hivyo, havitakuwa imara, vitaendelea kubaki kama vilivyo kama hakuna hatua za makusudi za kuvifanya vipige hatua kwenda mbele," anasema.

Kamanda huyo mstaafu anasema, hakuna chama chenye uchumi imara kama CCM ambayo inaonekana kuwa imara tangu kuanzishwa kwake huku kikifanikiwa kumaliza migogoro ndani bila athari mbaya.

"Ushauri wangu kwa vyama vya siasa hasa upinzani, ni kuwa na nidhamu ya dhati, kwani kama haipo, wanachama na viongozi hawasikizani. Suluhu pekee ya ya kuondoa migogoro ni nidhamu, kuvumiliana na kusikilizana,"anasema.

JUKWAA LA VIONGOZI

KUELEKEA AGOSTI 9

# Ndivyo historia uongozi wa kabila moja Kenya inavyoelekea ukingoni

**Na Damian Mnyikwa**

NI AGOSTI 9 Wakenya wanaingia kwenye sanduku la kura kuamua kama ni Mzee Tinga (Raila Odinga), anayeingia Ikulu au Makamu wa Rais William Ruto, anayekuwa rais wao.

Zikiwa zimesalia siku 20, jicho linaelekezwa kwenye uchaguzi huo ambao ni gumzo pengine kila kona ya Afrika Mashariki.

Charles Kayoka, mchambuzi wa siasa na mwanadiplomasia, anasema kuna jambo muhimu ndiyo maana Ikulu ya Kenya inamtaka Odinga.

Anasema licha ya sababu za kiutendaji ndani ya serikali kuchangia Uhuru Kenyatta kutomuunga mkono Ruto na kumgeukia hasimu wake Odinga, kuna jambo jingine wengi hawajalitambua.

"Jaramagi Odinga baba wa Odinga, Tom Mboya na Wakenya wengine wasio Wakikuyu, walinyimwa nafasi za juu za uongozi kutokana na sababu za ukabila." Anasema.

Anaongeza kuwa kwa muda mrefu Wakikuyu anakotoka Uhuru wanaamini kuwa wanapaswa kuendelea kuwa marais wa taifa hilo kwa madai kuwa waliifia nchi kwenye harakati za uhuru hasa Vita vya Maumau.

Aidha, walikuwa na ahadi za kurithishiana madaraka mathalani Jomo Kenyatta alimwambia Daniel Arap Moi ahakikishe Uhuru anakuwa rais na ndivyo ilivyokuwa.

Hivyo huenda pia rais Uhuru anamuunga mkono Odinga kama sehemu ya fadhila kwa urafiki wa wazazi wao, anasema Kayoka.


"Jambo la pili siasa za ukabila, kwa mara ya kwanza Wakikuyu wanakosa mgombea anayepewa nafasi ya kuibuka mshindi kwenye urais. Swali ambalo wengi wanajiuliza hii inaweza kuwa mwanzo wa safari ya kumaliza siasa za ukabila Kenya?" anahoji Kayoka.

Profesa Kitojo Watengere mchumi na mchambuzi wa siasa kutoka Chuo cha Diplomasia, anasema bado safari ni ndefu kumaliza siasa za ukabila nchini humo na wala jambo hilo halitoshi kuashiria. "Inawezekana ni jambo ambalo limetokea tu, lakini siamini kwamba linaonyesha ukabila umekwisha" Profesa Watengere.

Hata hivyo, kuna dhana inayopingana na maoni hayo kuwa jambo hilo si sawa na huwezi kusema jamii ya Wakikuyu haijapewa nafasi ya kukaribia uongozi ilhali Raila Odinga Mjaluo, amemteua mgombea Mwenza Martha Karua Mkikuyu na Ruto Mkalenjini mgombea mwenza wake ni Rigathi Gachagua Mkikuyu pia.

Hii inamaanisha kuwa kwa vyovyote vile iwe Raila Odinga ama William Ruto makamu wake atakuwa Mkikuyu.

"Hakuna angeweza kuthubutu kumchagua mgombea mwenza kutoka jamii nyingine maana ukifanya hivyo na unatafuta urais utakuwa umejitia kamba shingoni" anasema Benson Wakoli mchambuzi kutoka Nairobi, anayezungumza na Nipashe.



Makamu wa Rais William Ruto (kushoto) , Rais Uhuru Kenyatta na Raila Odinga (kulia), ndiyo wanaotikisa Kenya, wakati taifa hilo likielekea kwenye uchaguzi mkuu mwanzoni mwa mwezi ujao. **PICHA MTANDAO**

> Ruto ni kijana na ana safari ndefu ya kulitumikia taifa kuliko mtu ambaye ana miaka 77 ana muda mfupi sana wa kuongoza nchi na hawezi kutawala mihula miwili labda alazimishe.

Siasa za ukabila bado ni tishio kwa Kenya, Wakikuyu kabila kubwa bado wanataka kuhodhi madaraka. Wanaamini kuwa ndiyo wanapaswa kuwa katika mamlaka za juu za uongozi.

Haya ni madhara ya ukoloni ambayo waliyaweka makabila machache utawala na uongozi na mengine yakabakia katika ngazi ya utumishi, Charles Kayoka anasema.

Anataja changamoto hii kama mwiba kwa Afrika, mathalani Somalia ambapo ukoo na makabila machache ndiyo yana haki kikatiba kumchagua rais.

Anasema licha ya Tanzania kujitahidi kuondoa ukabila na mgombea yeyote kuingia madarakani, suala la ukanda lipo.

Kwa mfano, mgombea hawezi kutoka mkoa mwingine mathalani Arusha na kwenda Katavi kugombea ubunge bila kuwa mkazi wa eneo hilo, sio rahisi akubaliwe.

Kulingana na maoni ya wachambuzi hao licha ya Wakikuyu kutokuwa katika msitari wa mbele kugombea urais mwaka huu,bado wana nafasi kubwa kuendelea kutawala kwani watakuwa katika nafasi ya makamu.

Lakini je siasa ya Kenya ni mfano wa demokrasia Afrika Mashariki? Licha ya ukabila na changamoto kadhaa, uchaguzi wa Kenya unadhihirisha ukuaji wa demokrasia ikilinganishwa na wanachama wengine wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, anaongeza Kayoka.

Anataja hatua ya Makamu wa Rais Ruto, kutangaza kugombea urais kibishi kinyume na matakwa ya Rais Kenyatta, akisema ni ishara ya uhimilivu wa kisiasa.

"Kilichonifurahisha ni kuona kiongozi aliye madarakani anapingwa na mwenzake na hakuna matatizo" anaongeza Kayoka.

Akiunga mkono, Profesa Watengere, anasema demokrasia ya Kenya imeimarika zaidi kutokana na uwazi kwenye harakati za masuala ya siasa na uelewa mkubwa wa mambo.

Mchambuzi Wakoli naye anasema amekuwa mfuatiliaji mkubwa wa siasa ya Afrika Mashariki, akifuatilia uchaguzi wa Rwanda 2017 Tanzania na Burundi 2020, Uganda 2021 na Somalia 2022, na kuona kuwa Kenya kuna hatua kadhaa zimepigwa mbele kudumisha demokrasia.

"Wagombea wa upinzani serikali haina tatizo nao inawapa ulinzi na kuwafanyia kila kitu, haiwazuii kufanya mkutano mahali popote kinyume na mataifa jirani utashuhudia wagombea wa upinzani wanalalamika sana, Bobi Wine alikuwa analalamika wafuasi wake wanakamatwa vilevile kule nchini Burundi, Agathon Rwasa alikuwa analalamika kwamba serikali inanyanyasa wafuasi wake,wakati Kenya upinzani una uhuru wa kufanya chochote" anasema Wakoli.

### VIPI USHINDI?

Kati ya William Ruto na Raila Odinga nani atashinda? Wanapoulizwa swali hili, Profesa Watengere anasema mchuano ni mkali na katika kampeni zao wanavuta wafuasi wengi hasa vijana. Hivyo mzani umelala katikati, wawili hao wana uzito sawa kuibuka rais.

Wakoli anaona kitendawili kigumu kukitegua, ingawa anakiri kuwa kura za maoni zinaonyesha Odinga anaongoza kila kukicha lakini hii si mara ya kwanza kwake, kwenye uchaguzi uliopita aliongeza na hakuibuka mshindi.

Hivyo anaona ingawa Odinga anaungwa mkono na utawala lakini pia Ruto ana wafuasi wengi vijana ambao ndiyo wapiga kura.

Charles Kayoka, anampa nafasi kubwa Odinga kuibuka mshindi kutokana na uzoefu wake katika siasa ingawa anakiri kuwa angekuwa mkenya angeweza kumpigia kura Ruto. Sababu anazozitaja hasa ni suala la umri .

"Ruto ni kijana na ana safari ndefu ya kulitumikia taifa kuliko mtu ambaye ana miaka 77 ana muda mfupi sana wa kuongoza nchi na hawezi kutawala mihula miwili labda alazimishe," Kayoka anasema.

Anasema athari ya rais mzee kuongoza nchi ni kukosa nguvu ya kufanya maamuzi na badala yake walio chini yake kujiamulia wenyewe na kusababisha adha kwa raia.

Anatoa mfano raia wa Cameroon Paul Biya mwenye miaka 89, ambaye muda mwingi yuko Ulaya kutibiwa baada ya kudhoofika.

Kayoka anasema wale wanaomzunguka Biya ndiyo wanaoongoza na hilo anaamini linaweza kutokea kwa Odinga.

Wakenya wanatarajia nini kwa mshindi wa kiti cha urais? Mgombea yeyote atakayeibuka na ushindi katika kiti cha urais ana kazi kubwa ya kufanya kuyagusa maisha ya Wakenya wakati huu ambao uchumi wa taifa hilo uko katika hali mbaya kutokana na athari za UVIKO 19 na vita kati ya Ukraine na Russia, Profesa Watengere, anasema.

Anasema rais ajaye ana kazi kubwa ya kufanya kutokana na hali mbaya kiuchumi duniani, akitoa asilimia 50/50 kwa Odinga na Ruto kufufua uchumi kwa kile anachokieleza kuwa wamekuwa na sera zinazofanana.

Sera za wapinzani na serikali hazitofautiani sana kwa kuwa mara nyingi wakosoaji huangalia zaidi udhaifu wakiutumia kama chambo cha kuwabana kisiasa.

Wakoli anaamini kuwa yeyote atakayechukua silaha za uongozi katika uchaguzi wa mwaka huu ana kazi kubwa, mfano matatizo yanayowakabili Wakenya ikiwamo kupanda gharama za maisha pamoja na deni la taifa kuongezeka kwa viwango vya juu.

Wakenya wanaamini kuwa iwapo kiongozi atakayepatikana atajali masilahi yao kitu cha kwanza ambacho anatakiwa kufanya ni kudhibiti makali ya maisha na deni la taifa

"Jingine ni dondandugu la rushwa ambalo linalitafuna taifa rushwa inamaliza taifa, chohote unachotaka kufanya iwapo hutatoa rushwa basi hautakipata," anasema Wakoli .

Macho na masikio ya wana Afrika mashariki hasa wapenzi wa siasa yapo nchini Kenya taifa linalotajwa kuwa limestawi kidemokrasia ikilinganishwa na wana Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kenya mgombea atakayekubalika na wananchi ana nafasi kubwa ya kutwaa madaraka kwani si ajabu chama tawala kuangushwa na kuingia kwenye upinzani tofauti na mataifa mengine ya ukanda huo.



# TAKUKURU yaandaa vijana kuikabili rushwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Dodoma imesema itahakikisha shule za sekondari na msingi mkoani humo zinakuwa na klabu za wapinga rushwa, ili kuwajengea uelewa vijana tangu awali.

Mkuu wa TAKUKURU mkoani Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alibainisha hayo juzi alipozungumza na Nipashe kuhusu utoaji elimu ya kupiga vita rushwa katika maeneo mbalimbali.

Alisema klabu za wapinga rushwa shuleni zinasaidia kwa kiasi kikubwa wanafunzi kujua umuhimu wa kuzuia rushwa, ikiwamo kutambua haki zao za msingi pale wanapokumbana na vitendo vya rushwa.

Kibwengo alisema wamekuwa wakishirikiana na walimu walezi wa klabu hizo katika shule mbalimbali za msingi na sekondari zilizomo mkoani mwake kuhakikisha elimu hiyo inawafikia wanafunzi shuleni ili wakawe mabalozi wazuri wanapohitimu masomo yao.

"Tumekuwa tukijitahidi kushirikiana na walimu walezi wa klabu za kupinga rushwa katika shule, tunahitaji kuona wanafunzi wanatambua madhara ya rushwa wangali watoto wadogo," alisema.

Kibwengo aliwataka wanafunzi waliopo kwenye klabu hizo, wasome kwa bidii ili baadaye taifa liwe na wataalamu wazuri ambao wataongoza vitengo mbalimbali pindi watakapohitimu elimu ya juu.

Alisema wamekuwa wakiwasisitiza hata pale wanapohitimu, wakawe mabalozi wazuri katika maeneo wanayoishi na hata kutoa elimu kwa wale wasio na upeo wa madhara yatokanayo na rushwa.

Vilevile, alisema klabu hizo za wapinga rushwa kama mabalozi, kazi yao ni kutoa elimu kwa jamii, pia kufuatilia miradi ya maendeleo inayotekelezwa na serikali ikiwamo kuhoji ili kusaidia kuiokoa kama watekelezaji wanakwenda kinyume.

Aliwasisitiza kuwa wao kama viongozi watarajiwa, jukumu lao ni kusoma kwa bidii na wazalendo wa kushiriki kikamilifu katika kupinga rushwa.

Alisema taasisi hiyo itakuwa ikiandaa mashindano mara kwa mara ya kujadili mada za kupinga vitendo vya rushwa ikiwamo namna ya kuzuia, ili kuzidi kuchochea uelewa kwa wanafunzi kuhusu kupiga vita rushwa katika maeneo mbalimbali.

# Sauti ya JPM ilivyotumika kutatua mgogoro wa maji

**Na Paul Mabeja,** MPWAPWA

SAUTI ya Hayati Dk. John Magufuli, Rais wa awamu ya tano, imetumika kutatua mgogoro wa maji kati ya wakazi wa Kijiji cha Mtera na Meneja wa Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) wilayani Mpwapwa.

Kutumika kwa sauti hiyo kulitokea baada ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Antony Mtaka, kufanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi wa maji wa Sh. bilioni 1.7 unaotekelezwa na wakala huo.

Ilielezwa katika ziara hiyo kuwa mradi huo ni matokeo ya ziara ya Hayati Magufuli aliyoifanya katika kijiji hicho na kuagiza RUWASA kupeleka huduma ya maji katika kijiji hicho ambacho kilikuwa kinakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji.

Husein Mkwizu, mmoja wakazi wa kijiji hicho, alisema kuwa enzi za uhai wake, Rais Magufuli alipita katika kijiji hicho na kuzungumza na wananchi ambao walimlalamikia kuwa hawana huduma ya majisafi na salama.

"Alipita hapa Hayati Rais Magufuli na kuzungumza na wananchi na sisi tukamweleza kuwa hatuna huduma ya majisafi na salama kwani tulikuwa tunatumia maji ya chumvi ambayo hayafai kwa matumizi ya binadamu.

"Na alipouliza ikabainika kuwa wenzetu wa TANESCO (Shirika la Umeme) hapo jirani na kijiji wanakunywa maji baridi na salama kutoka katika bwawa linalotumika kufua umeme.

"Kutokana na hali hiyo, Hayati Rais Magufuli aliwaagiza TANESCO kuhakikisha kuwa maji wanayoyatumia kutoka kwenye bwawa na sisi wananchi tupatiwe bure na waendelee kutupatia huduma hiyo hadi pale mradi wetu utakapokamilika," alilisitiza Mkwizu.

Alisema kuwa kutokana na maagizo hayo, TANSESCO walitekeleza kupitia meneja wake wa mkoa kuanza kuwapatia huduma hiyo bure kama walivyoagizwa na mkuu wa nchi huyo wa wakati huo.

"Tulianza kupatiwa huduma ya maji kutoka TANESCO bure wakati RUWASA wakiendelea kutekeleza maagizo mengine yaliyotolewa na kiongozi huyo wa nchi lakini sasa tunashindwa kuelewa kabla ya mradi wetu kukamilika wamesitisha ule mradi wa TANESCO uliokuwa ukitupatia maji.

"Huu mradi wa RUWASA bado kabisa haujakamilika lakini leo hii wanadai upo katika asilimia 75 na wamekata ule wa TANESCO wakati walikuwa wako tayari kuendelea kutupatia maji kama walivyoagizwa," alilalamika.

Meneja wa RUWASA Wilaya ya Mpwapwa, Cyprian Warioba, akijibu malalamiko hayo ya wananchi mbele ya mkuu wa mkoa, alilazimika kutumia sauti ya Dk. Magufuli iliyorekodiwa ili kujibu hoja hizo za wananchi.

Baada ya kuicheza sauti hiyo kwenye spika na kila mmoja kusikiliza maagizo ya Rais Magufuli kipindi hicho, ndipo akaanza kujibu hoja kuwa malalamiko ya wananchi siyo ya kweli.

"Maagizo yalikuwa hivi, lazima niseme ukweli, msema ukweli ni mpenzi wa Mungu. Magufuli alisema TANESCO wafunge bomba moja nje ili wananchi wapate maji lakini kulikuwapo na msongamano, hivyo tukalazimika kuleta maji kwenye mfumo wa kwanza uliokuwa unatumika kwenye mradi wa maji chumvi na sasa bado tunaendelea jitihada zingine," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mtaka, alitoa siku 60 kwa RUWASA kukabidhi mradi huo wa maji ili wananchi waanze kupata huduma hiyo ya majisafi na salama.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweli (wa pili kushoto), akizungumza na watumishi wa ngazi ya waratibu elimu, maofisa elimu na walimu wakuu katika semina elekezi ya kuwaandaa kwa ajili ya usaili wa makarani wa sensa ya watu na makazi, wilayani humo jana. Kushoto ni Mratibu wa Sensa ya Watu na Makazi wa Jiji la Dodoma, Calista Makacha. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# OSHA yasisitiza kuboresha mazingira kuvutia uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAKALA wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) umesisitiza nia yake ya kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara nchini kupitia uimarishaji wa mifumo ya usalama na afya mahali pa kazi ili kuwafanya wawekezaji wajisikie fahari kuwekeza nchini.

Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alibainisha hayo jana wakati akifungua kikao kazi cha siku tano jijini Dodoma kilichowakutanisha wakaguzi wa afya wa OSHA kutoka maeneo mbalimbali nchini.

"Wote tunaona mwelekeo wa serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan inavyosisitiza kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji na kufanya biashara nchini.

"Hivyo, kupitia kikao kazi hiki, sisi OSHA ambao ni taasisi wezeshi, tunaangalia ni namna gani ambavyo tunaweza kuwezesha mazingira ya uwekezaji na baishara nchini yakawa ni rafiki zaidi, hivyo kuwafanya wafanyabiashara na wawekezaji wajisikie fahari kuwekeza nchini.

"Tumekaa na timu ya madaktari wa OSHA wapatao 100, nia na madhumuni ni kuhakikisha tunatoa huduma bora na kwa wakati, pia tunaangalia ni namna gani tutawezesha maeneo ya kazi nchini yaweze kusimamia Sheria Na. 5 ya Usalama na Afya Mahali Pa Kazi ya Mwaka 2003," alifafanua.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo, Shirika la Kazi Duniani (ILO) katika siku za hivi karibuni limepitisha azimio la kila nchi mwanachama ahakikishe anasimamia kikamilifu masuala ya usalama na afya kazini, jambo ambalo limeisukuma OSHA kujipanga kutimiza azimio hilo.

Wakaguzi wa afya wa OSHA walisema kuwa baada ya kikao kazi hicho, watakuwa na maono ya pamoja katika kuboresha mazingira ya kazi nchini huku wakitoa wito kwa waajiri kusimamia ipasavyo Sheria Na. 5 ya Usalama na afya Mahali pa Kazi ya Mwaka 2003 ili kuleta tija katika uzalishaji.

"Kupitia kikao kazi hiki tutatoka na maazimio ya pamoja yatakayotuongoza katika kuboresha mazingira ya kazi, hivyo kila mmoja wetu akitoka hapa, atakuwa anajua malengo ya taasisi ni yapi.

"Mathalani tunahitaji kuwafikia watu wangapi na tutafanya kazi kwa kiasi gani katika mwaka mpya wa fedha wa 2022/23," alisema Dk. Denis Gabriel, Mkaguzi wa Afya wa OSHA.

Blandina Reuben, Mkaguzi wa Afya wa OSHA, aliwataka waajiri kusimamia ipasavyo sheria na miongozo mbalimbali ya usalama na afya mahali pa kazi ili kuleta tija katika uchumi wa nchi.

"Nitoe wito kwa waajiri wote katika maeneo mbalimbali ya kazi wazingatie Sheria Na. 5 ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi ya Mwaka 2003 kwa sababu sheria hiyo ikizingatiwa ipasavyo, inampunguzia gharama mwajiri na kuongeza tija katika eneo la kazi," alisema Blandina.

Kikao kazi hicho kinafanyika kwa lengo la kutathmini utendaji kazi wa taasisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/22 pamoja na kupitia miongozo na kanuni mbalimbali za afya mahali pa kazi ili kuendelea kuboresha utendaji kazi wa taasisi hiyo.



# Tanzania yatajwa kuwa na ardhi uzalishaji mazao tofauti

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WADAU wa utafiti wa mazao kutoka katika mataifa sita duniani, wamesema Tanzania ni nchi pekee katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati yenye ardhi inayofaa kwa uzalishaji wa mazao mbalimbali ya aina tofauti.

Aidha wamesema Tanzania ina uwezo wa kuzalisha chakula cha kutosheleza bara zima la Afrika na ziada kuuzwa katika mabara mengine endapo wakulima watawezeshwa teknolojia na zana za kisasa za kulimia.

Wadau hao ni kutoka katika mataifa ya Marekani, Uholanzi, Hispania, Kenya, Rwanda na Uganda waliyasema hayo walipotembelea Kituo cha Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Uyole jijini Mbeya kwa ajili ya kufuatilia uzalishaji wa mbegu bora za maharagwe.

Wadau hao ni watafiti wa mazao ya maharagwe, mbaazi, kunde, karanga na ulezi ambayo ni miongoni mwa yanayostawi katika maeneo mbalimbali nchini.

Mmoja wa wadau hao, Chriss Ojiewo ambaye ni Mratibu wa Mradi wa AVISA unaohusika na mazao hayo, alisema Tanzania ndilo taifa katika ukanda wa Afrika Mashariki lenye eneo kubwa linalofaa kwa kilimo.

Alisema katika mataifa mengine ardhi haifai kwa kilimo na hata maeneo ambayo yanafaa ni kwa mazao machache na mengi yanategemea zaidi kupata chakula kutoka Tanzania.

Alisema kutokana na hali hiyo wanaamini kwamba endapo ardhi yote ya Tanzania itatumika vizuri, kuna uwezekano ikawa na uwezo wa kulisha bara zima la Afrika. "Ukiangalia hii nchi inazalisha kila aina ya zao tofauti na mataifa mengine, lakini pia ina mabonde yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na hata kilimo cha kutegemea mvua, kinachotakiwa kwa wananchi ni elimu pekee," alisema Ojiewo.

Naye Mjumbe wa Mradi wa AVISA kutoka Uganda, Clea Mugisha, alisema shirika hilo linajihusisha na uendelezaji wa mazao mbalimbali na waliamua kutembelea taasisi hiyo ili kueneza zaidi teknolojia.

Alisema moja kati ya mazao wanayoyalenga ni maharagwe ambayo kwa sasa yanahitajika katika maeneo mbalimbali duniani na kueleza kwamba wanataka kuwekeza zaidi nguvu kwenye uendelezaji wa teknolojia.

Alisema wanatafiti zaidi wa mazao hayo kwa lengo la kujua mahitaji halisi ya soko, uzalishaji ulivyo pamoja na kuwatafutia wakulima masoko ili kuendeleza mazao hayo.

"Tunalenga zaidi kuwanufaisha Watanzania kwenye mradi huu, lakini kilichotuleta zaidi kwenye taasisi hii ni zao la maharagwe ambalo limefanyiwa utafiti vizuri na taasisi hii, wamezalisha aina mbalimbali za maharagwe hapa," alisema Clea.

Mbobezi wa utafiti wa maharagwe nchini ambaye pia ni Mkurugenzi wa Kituo cha TARI Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema serikali imewekeza fedha nyingi kwenye utafiti wa mazao.

Alisema katika kituo hicho wamezalisha mbegu mbalimbali za maharagwe ambazo nyingi zinazaa kwa wingi na zina uwezo wa kuzaa gunia 10 kwa ekari moja.



Mratibu wa Sensa ya Watu na Makazi wa Mkoa wa Mbeya, John Lyakurwa (kulia), akitoa maelekezo kwa wakufunzi wa makarani wa sensa katika Kata ya Iwindi, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi jana, wakati wa mafunzo ya matumizi ya vitendea kazi vikiwamo vishikwambi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wahakikishiwa eneo ujenzi Chuo Kikuu MCHAS

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI ya Mkoa wa Mbeya, imesema inaendelea na mchakato wa kulipata eneo la mashamba ya Kiwanda cha Tanganyika Packers lililopo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi kwa ajili ya ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Ndaki ya Afya na Sayansi Shirikishi (MCHAS).

Eneo hilo ambalo kwa sasa linatumika kwa ajili ya kilimo linaelezwa kuwa na ukubwa wa hekta 600 na linahitajiwa na chuo hicho kwa ajili ya ujenzi wa ndaki ya afya na sayansi shirikishi pamoja na hospitali ya kufundishia.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliyasema hayo juzi wakati wa kongamano la kuadhimisha miaka 60 ya chuo hicho kuwa lengo la serikali ni kuhakikisha mradi huo unaanza kujengwa mwakani.

Homera alisema wanaendelea kuwasiliana na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba pamoja na viongozi wengine wa serikali kuhusu njia sahihi ya kulitwaa eneo hilo mapema na kuanza ujenzi.

Alisema mradi huo ni muhimu kwa maendeleo ya mkoa huo na kusisitiza kuwa hawawezi kuruhusu ndaki hiyo kuhamishiwa katika mkoa mwingine.

"Lengo letu ni kuhakikisha mradi huu unaanza kujengwa mapema mwakani, lile eneo ni kubwa na linafaa kwa ajili ya kujenga taasisi kubwa kama hizi kwa hiyo niwahakikishie kwamba mpaka sasa tumefikia hatua nzuri sana ya kulipata," alisema Homera.

Awali, Mkuu wa Ndaki ya MCHAS, Prof. Projestine Mganyizi, alisema walianza kuliomba eneo hilo kwa muda mrefu, lakini kwa sasa wameanza kupata matumaini baada ya Mkuu wa mkoa kuwahakikishia.

Alisema wanahitaji kujenga mradi huo ambao ni mwendelezo wa mafanikio chuo hicho kuasisi hospitali mbalimbali ikiwamo Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na kwamba kwa Mbeya wanahitaji hospitali kubwa ya kufundishia.

Alisema katika kipindi hiki cha kuadhimisha miaka 60 ya kuanzishwa kwa chuo hicho miongoni mwa matunda ambayo wanajivunia ni pamoja na kuwa na viongozi wengi wa kitaifa waliosoma katika chuo hicho.

Prof. Mganyizi aliwataja baadhi ya viongozi wa kitaifa waliosoma katika chuo hicho kuwa ni pamoja na Rais mstaafu wa awamu ya nne, Dk. Jakaya Kikwete, ambaye kwa sasa ndiye Mkuu wa chuo hicho.

"Tunapoadhimisha miaka 60 ya chuo chetu tunahitaji kuweka alama katika maeneo tofauti ya nchi, sasa kwa Mbeya lengo letu ni kupata eneo la kujenga hospitali, lakini kwa muda mrefu tumekuwa tukilitafuta bila mafanikio," alisema Prof. Mganyizi.

Alisema kwa sasa baada ya serikali kutangaza kuanza mikakati ya kukipatia chuo hicho eneo, watahakikisha wanalitumia kujenga chuo cha kisasa na hospitali ya kisasa ya kufundishia.

Mwaka 2021, Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Kikwete alitahadharisha kuwa endapo Serikali ya Mkoa haitakipatia chuo hicho eneo lenye ukubwa wa ekari 500 watakihamishia katika mkoa mwingine ambao utakuwa tayari.

## Vifaa vya kisasa kutumika katika Sensa ya Watu na Makazi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MRATIBU wa Sensa ya Watu na Makazi wa Mkoa wa Mbeya, John Lyakurwa, amewataka wananchi wa mkoa huo kujitokeza kuhesabiwa Agosti 23, mwaka huu na kutoa taarifa sahihi ili kuliwezesha taifa kupata takwimu sahihi.

Aliyasema hayo jana alipozungumza na wandishi wa habari kuhusu maandalizi yake katika mkoa huo na kwamba kwa sasa wanaendelea kutoa mafunzo kwa maofisa wa sensa watakaokuwa wanakusanya takwimu kwa wananchi.

Alisema kwa sasa wameanza kufanya mazoezi ya kuvijaribisha vifaa vitakavyotumika kwenye sensa hiyo vikiwamo vishikwambi ili kuhakikisha kama vina fanya kazi ipasavyo.

Alisema wamefanya zoezi hilo kwa muda mrefu kutokana na teknolojia inayotumika kwa sasa kuwa mpya tofauti na iliyokuwa inatumika katika sensa za miaka ya nyuma ambazo walikuwa wanatumia makaratasi.

"Ninachowataka wananchi wa Mkoa wa Mbeya ni kuhakikisha wanajitokeza siku hiyo na kutoa taarifa sahihi, nawaomba wasiwafiche watoto wa aina yeyote wakiwamo wenye ulemavu, hapa ukiangalia pia hata hawa wenye ualemavu tumewashirikisha," alisema Lyakurwa.

Alisema teknolojia inayotumika kwa sasa ya kutumia vishikwambi ni bora zaidi kutokana na kufanya kazi haraka na kuwasaidia maofisa kupeleka taarifa kwa haraka zaidi.

Alisema maofisa watakaoshiriki kwenye sensa wamepata mafunzo ya matumizi ya vishikwambi hivyo na kwa sasa wanafanya nao majaribio ili waendelee kupata uzoefu kabla ya siku kufika.

Nao baadhi ya maofisa wa sensa walioshiriki kwenye mafunzo hayo kwa vitendo walisema teknolojia hiyo ya kutumia vishikwambi itawarahisishia kazi tofauti na kutumia makaratasi.

Mmoja wa maofisa hao, Khatib Luga, alisema teknolojia ya kutumia vishikwambi itawasaidia kukusanya takwimu kwa wakati na kuzituma mapema.

Alisema walipata mafunzo ya awali kuhusu matumizi ya vifaa hivyo na kwa sasa wamepelekwa mitaani kwa ajili ya kuangalia ufanisi wake kabla ya kuelekea kwenye zoezi hilo muhimu.





## Waziri aona fursa utalii wa matibabu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale, Simai Mohamed Said, amesema wakati umefika kwa sekta binafsi kujikita zaidi katika ujenzi wa hospitali zenye hadhi kwa ajili ya kutoa huduma za afya kwa watalii.

Aliyasema hayo jana katika kongamano la kuimarisha sekta ya afya lililofanyika mjini Zanzibar, akisisitiza kuwa Zanzibar imeruhusu uwekezaji wa ujenzi wa hoteli kubwa zenye hadhi ya juu.

Waziri huyo alisema mikakati na malengo hayo yanatakiwa kwenda sambamba na ujenzi wa hospitali zitakazotoa huduma kwa watalii wa daraja la juu.

Alisema hadi sasa hakuna huduma za matibabu ya juu kwa watalii wanapopata matatizo mbalimbali kuhusu afya zao ambapo wakati mwingine hulazimika kusafirishwa kwenda Nairobi, Kenya.

Alisema kuwapo kwa uwekezaji katika sekta binafsi katika masuala ya afya kwa kiasi kikubwa kutasaidia kuleta mapinduzi makubwa yatakayoleta ufanisi katika sekta hiyo.

"Sekta ya utalii imepewa kipaumbele ambacho inachangia kwa asilimia 49 katika mapato ya nchi na kwa sasa tunahitaji ushiriki wa sekta binafsi katika ujenzi wa hospitali zenye hadhi zitakazotowa huduma ya afya kwa wageni," alisema.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema mikakati ya serikali ni kuona kasi ya ujenzi wa hospitali zenye ubora na hadhi ya kutoa huduma kwa wananchi.

Alisema wakati kasi ya ujenzi wa miradi ya hoteli za kitalii ukiendelea, ujenzi wa hospitali zenye hadhi ya juu unahitajika ili kwenda sambamba na utoaji wa huduma bora kwa wageni.

Alisema Wizara ya Afya inatekeleza mradi wa ujenzi wa hospitali 10 za wilaya Unguja na Pemba ambazo zitakapomalizika zitakuwa na uwezo mkubwa wa kufikisha huduma kwa wananchi.

Alisema mikakati ya wizara ni kukaribisha sekta binafsi inatekeleza miradi ya ujenzi wa hospitali zenye hadhi na uwezo mkubwa wa kuhudumia watalii.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi (ZIPA), Sharif Ali Sharif, alisema wanakaribisha maombi ya uwekezaji katika miradi ya ujenzi wa hospitali za kisasa zitakazotoa huduma za afya kwa wageni.

Alisema uwekezaji huo ni muhimu kufuatia kuongezeka kwa kasi ya miradi ya hoteli za kitalii za kisasa ambao unatakiwa uende sambamba na upatikanaji wa huduma za afya zenye ubora.

# Rais Mwinyi aagiza taka zitumike kuzalisha umeme

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema ili kudhibiti uchafu wa kuzagaa kwa taka katika Mji wa Zanzibar, lazima taka zitumike kwa matumizi mbadala ikiwamo umeme utokanao na taka.

Aliagiza hayo jana kwenye Ukumbi wa Shekhe Idrisa Abdulwakil mjini Zanzibar wakati wa majumuisho ya ziara yake ya kukagua miradi ya maendeleo katika Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Alisema bado kuna tatizo la kuzagaa kwa taka katika mkoa huo, hivyo ni vyema zikatumika kwa matumizi mazuri na kuleta maendeleo badala ya kuzagaa mitaani na kuchafua madhari ya mji.

"Lazima taka hizi zilizozagaa tuzitumie vizuri, upo uwezekano wa kuzitumia taka kwa ajili ya kuzalisha umeme," Dk. Mwinyi aliagiza.

Alisema endapo hatua hiyo ikifanikiwa, tatizo la kuzagaa kwa taka litaondoka na mji utaimarika kwa kuwa safi na kuzidi kuwa kivutio kwa wageni wanaofika Zanzibar.

Alisitiza umuhimu wa manispaa kupambana na tatizo la uchafu katika maeneo mbalimbali ya barabara na maeneo ya mji, hususan maeneo ya ndani, huku akisisitiza azma ya serikali ya kuzibadili taka kuwa rasilimali zenye thamani. Kuhusu huduma ya majisafi na salama, Dk. Mwinyi alisema hajaridhishwa na upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama katika mkoa huo.

Alisema kuna kero kubwa ya upungufu wa upatikanaji wa huduma hiyo, hali ambayo imezusha manung'uniko ya wananchi kukosa huduma hiyo muhimu.

Aliitaka Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kuhakikisha mkoa wote unapata huduma hiyo muhimu na kuwaondolea mzigo mzito wananchi kutafuta huduma ya maji.

Dk. Mwinyi pia aliiagiza Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) kufanya uchunguzi ili kubaini namna mkandarasi wa kampuni ya ujenzi ya Associated Investment Company Limited alivyopata kazi ya ujenzi wa Shule ya Sekondari Mtopepo.

Alisema katika mradi huo, mkandarasi huyo amebainika hana uwezo, hivyo kuna umuhimu wa ZAECA kufanya uchunguzi ili kubaini namna alivyopata kazi hiyo kwa kuwa kuna shaka kuwa huenda alipata kazi hiyo baada ya kuweka kiwango cha chini cha gharama za ujenzi au mbali na kujulikana kuwa hana uwezo, alipewa kazi hiyo baada ya kutoa rushwa.

Katika ziara yake hiyo, Dk. Mwinyi pia alibaini shida katika ujenzi wa masoko, hivyo akaitaka sekta binafsi kuwa na uhakika wa uwezo wa makandarasi kabla ya kuwapa miradi.

Alisema serikali imefanya uamuzi wa kuendeleza mradi wa ujenzi wa masoko ya Jumbi, Mwanakwerekwe na Chuini kwa kukitumia Kikosi cha Kujenga Uchumi (JKU) baada ya kugundua kuwa sekta binafsi imeshindwa kukamilisha miradi hiyo kwa wakati.

Vilevile, alizitaka idara za manispaa kuweka fedha za kutosha katika kuendeleza miradi ya maendeleo kutokana na makusanyo wanayofanya.

Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi, Idrissa Kitwana Mustafa, mbali na kutoa shukrani kwa viongozi, watendaji na wananchi wa mkoa huo kwa kushiriki kikamilifu katika ziara hiyo, alisisitiza umuhimu wa wafanyabiashara na wananchi kutoa na kudai risiti wakati wanapofanya ununuzi.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akipanda mti baada ya kukagua kituo cha wajasiriamali Kijiji cha Pale Kinyongele, Mkoa wa Kaskazini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mkoa wapata dawa ya migogoro ya ardhi

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

KATIKA kuhakikisha jamii ya Mkoa wa Kaskazini Unguja inaondokana na migogoro ya ardhi, uongozi wa mkoa umefuatilia migogoro ya ardhi iliyoripotiwa katika wilaya zake na kuifanyia kazi.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, alibainisha hayo jana alipowasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo za mkoa huo kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Juni 2020 wakati Rais wa Zanzibar, Dk. Mwinyi alipozuru kukagua miradi ya maendeleo katika mkoa huo.

Ayoub alisema jumla ya migogoro 1,177 ya ardhi imeripotiwa ambapo 421 imetatuliwa na 756 iliyobakia, hatua za kuitatua zinaendelea kwa kushirikiana na kamisheni ya ardhi.

Alisema mkoa huo unaendelea kuwaelimisha wananchi juu ya hatua za kuchukua wakati wanapotaka kufanya uhaulishaji wa ardhi ili kuondoa uwezekano wa kutokea migogoro ya ardhi.

Kuhusu udhibiti wa mchanga, Ayoub alisema Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi (ZAECA) ilifanya udhibiti katima mashimo ya mchanga eneo la Pangatupu, Donge Muwanda na matokeo yake, tani 96,341 zilizoripotiwa kuchimbwa na kupatikana jumla ya Sh. milioni 667.076 zilizokusanywa na serikali kwa mwezi wa Januari mwaka huu.

"Baada ya udhibiti mwezi Februari mwaka huu, jumla ya tani 214,141 ziliripotiwa kuchimbwa na jumla ya Sh. bilioni 1.479 zilikusanywa.

Alisema ZAECA imefanya udhibiti katika Bandari ya Donge ambapo bandari hiyo hutumika kwa kuteremsha wanyama wanaotoka Tanzania Bara na kufanikiwa kuokoa jumla ya Sh. milioni 1.764 kwa mwezi Mei mwaka huu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

ORM 58

**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE**
**NO.............619......OF 2022**
**In the matter of the estate of the late...........**
**JOSEPH SALUM LUBUMA**
**and**
**In the matter of application for letters of administration by....RAHELI JOSEPH LUBUMA**

**GENERAL CITATION**
(Rule 75)

All persons claiming to have any interest in the estate of the above- named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the **23rd day of AUGUST 2022**
**Dated at DAR ES SALAAM this 13TH day of JULY 2022**

Registrar/Senior Resident Magistrate

---

MWAMBA AUCTION MART AND RECOVERIES
P.O.BOX 429 DODOMA – TANZANIA
OFFICE LOCATION: CCM REGIONAL BUILDING ROOM No. 9
0715170553 / 0756011439

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa Amri ya Mahakama ya Mwanzo Dodoma Mjini, nitauza kontena moja laa biashara lenye urefu wa futi 20 lililopo four ways Dodoma, mali ya Ndg. **DAMASI RAYMOND MBOYA**. Litauzwa ili kumlipa matalaki wake Bi **LUCY VICENT MWORIA** kutokana na shauri la madai namba 32 ya mwaka 2017. Mnada utafanyika tarehe 05/08/2022 kuanzia saa 4:00 asubuhi mahali kontena lilipo.

> Dalali ndiye mpiga nyundo wa mwisho.na mshindi atalipa fedha zote papo hapo
> Kontena litauzwa kama lilivyo
> Gharama za kuhamisha kontena hilo ni juu ya mnunuzi

**NB:ikiwa unahitaji kuliona kabla ya siku ya mnada, piga +255713 170 553**

---

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **CITI BANK TANZANIA ,Sepco Debt Collection & Auctioneering Co,Ltd** tutauza kwa mnada wa hadhara Jenereta **(GENERATOR)** iliyoko kwenye jeduali,mnada utafanyika **Tarehe 29/07/2022,** katika yard yetu iliyopo Tabata Kimanga kuanzia saa mbili asubuhi,

| SERIAL NO. | MODEL | CAPACITY |
|---|---|---|
| GD03-4559040 | CUMMINS-F10KBGS990 | KVA 55 |

**MASHART YA MNADA**
Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi,Genereta linauzwa kama liilivyo,Ukaguzi utaanza Tarehe 20/07/2022

**Mawasiliano piga:**
**0715-683777/0782548337**
**info@sepcoauctioneering.co.tz**
**www.sepcoauctioneering.co.tz**

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI

**DAVID LISA MWANILUNGA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 810 CPN** RANGI YA BLUU.YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/284320/2022**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HARRY JAMES MWANSEMBO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA SPACIO yenye usajili namba **T 838 BLM ,** CHASSIS NAMBA: **AE1116149504,** ENGINE NAMBA: **4AH892845.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/KIJ/RB/276150/2022**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JESSICA EVELYNE SANGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya VOLKSWAGEN yenye namba za usajili **T412 CJY,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DAR/CHA/RB/285500/2022**

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya Mwanzo Mikongeni**

**Usimamizi wa Mirathi NO.14/2022**

**Ombi la AZIZA JUMA KISALEKO Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu SALMA ISMAIL MOHAMED**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja kuhudhuria Kesi Wakitaka Mnamo tarehe 20/09/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi hiyo .
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 15/07/2022

SAINI YA HAKIMU
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MIKONGENI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa. DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na 42/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU SALUMU MWINYI HAMISI AKIDA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MWINYI HAMISI AKIDA**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 01 Mwezi 08 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo **Tarehe 18 Mwezi 07 Mwaka 2022**

HAKIMU
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
CHAMWINO-MJINI
DODOMA

---

## KUFUNGA KAMPUNI

WAMILIKI **EZEKIEL JAPHET SAGASII & CATHERINE JOSEPH MUOJERWA** WA KAMPUNI YA **REMIMA BUSINESS COMPANY LTD** YENYE USAJILI NO **133686** MNAMO TAREHE **30/03/2021**, WANAPENDA KUUTANGAZIA UMMA KUWA KAMPUNI YAO HAIJAKIDHI VIGEZO VYA BOT YA KUBADILI JINA LA BIASHARA LIWEZE KUSOMEKA MICROFINANCE HIVYO KUAMUA KUIFUNGA KWA MUJIBU WA SHERIA YA MAKAMPUNI BRELA

REMIMA BUSINESS CO LTD
P. O. BOX 220
DODOMA

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HAJI YUSUPH MACHA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **NISSAN CARAVAN** yenye usajili namba **T469 DFT,** CHASSIS NAMBA: **FEGE24002039** na ENGINE NAMBA: **OD32153424.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA **: ARU/ARU/RB/225386/2022**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**WINFRIDA ALBOGASTI MOSHA** ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya **BAJAJI (TVS-KING)** yenye namba za usajili **MC 709 CLN.** Chassis namba: **MD6M14PAOK4N11894.** Engine namba: **AK4NK4211894.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi RB namba **IRI/IRI/RB/276635/2022.**

---


**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Putin, Erdogan, Rais wakutana

**TEHRAN,** Iran

MARAIS Recep Tayyip Erdogan wa Uturuki, Ibrahim wa Iran na Vladimir Putin wa Russia, wanafanya mkutano utakaogubikwa na vita inayoendelea nchini Ukraine.

Rais Erdogan alipokelewa na Rais Ibrahim Uwanja wa Ndege wa Tehran asubuhi ya jana, wakati Rais Putin aliwasili tangu juzi, kwa mazungumzo ya kina juu ya vita nchini Syria.

Mataifa yote matatu yanahusika moja kwa moja kwenye vita hivyo vya Syria, Iran na Russia zinaunga mkono utawala wa Rais Bashar al-Assad, huku Uturuki ikiwaunga mkono waasi.

Mkutano huo wa pande tatu umejikita kuendeleza kile kiitwacho mchakato wa amani wa Astana unaodhamiria kukomesha vita vilivyodumu zaidi ya miaka 11 katika taifa hilo la Kiarabu.

**Kwa miezi kadhaa, rais huyo wa Uturuki amekuwa akipendekeza kukutana na Putin kwa lengo la kupunguza hali ya wasiwasi iliyozuka duniani kutokana na uvamizi huo.**

Mkutano huo wa kilele ni wa kwanza kuitishwa na Rais Ibrahim, tangu achukuwe madaraka mwaka jana na inakuwa safari ya pili kwa Rais Putin nje ya nchi tangu alipoamuru uvamizi nchini Ukraine mwezi Februari mwaka huu.

Mkutano huo unafanyika siku chache baada ya Rais Joe Biden wa Marekani kutembelea eneo la Mashariki ya Kati kwa mara ya kwanza tangu aingie madarakani.

Mkutano huu unafanyika baada ya Rais Erdogan wa Uturuki kutishia mwaka jana kwamba angefanya mashambulizi kaskazini mwa Syria dhidi ya wanamgambo wa Kikurdi, ambao inadai ni magaidi.

Hata hivyo, Iran ilishaionya kwamba hatua yoyote ya kijeshi ya Uturuki nchini Syria inaweza kuliingiza eneo zima kwenye mzozo mkubwa zaidi.

Ingawa mkutano huo hauhusiani na Ukraine, lakini utatowa nafasi kwa Erdogan kukutana kwa mara ya kwanza ana kwa ana na Putin tangu Russia ilipoivamia Ukraine mwezi Februari.

Kwa miezi kadhaa, rais huyo wa Uturuki amekuwa akipendekeza kukutana na Putin kwa lengo la kupunguza hali ya wasiwasi iliyozuka duniani kutokana na uvamizi huo.

**MKE WA ZELENSK AWASILI MAREKANI**

Mke wa Rais wa Ukraine, Olena Zelenska, yuko Marekani kwa ajili ya kufanya mikutano ya ngazi ya juu na kuhutubia Bunge la Congress.

Ziara yake inakuja miezi minne baada ya mume wake, Rais Volodymyr Zelensky, kutoa hotuba ya mtandaoni kwa Congress, akishinikiza kupata vifaa zaidi vya kijeshi.

Olena, alikutana na Waziri wa Mambo ya Nje Antony Blinken Jumatatu na anatarajiwa kufanya mazungumzo na mwenzake Jill Biden, Jumanne katika Ikulu ya White House.

Anatarajiwa kulihutubia bunge la Capitol Hill leo.

Mke huyo wa Zelenska alikutana na Samantha Power, mkuu wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Marekani.

Shirika hilo limetoa mabilioni ya dola kusaidia serikali ya Ukraine kwa mahitaji ya kibinadamu, pamoja na kufanya kazi ya kukabiliana na uhaba wa chakula duniani uliochochewa na vita vya Russia. **DW**



Mlinzi wa jengo la Malkia la Buckingha, nchini Uingereza, akipewa maji kutokana na nchi hiyo kukumbwa na hali ya joto kali. **PICHA: REUTERS**

## Ulaya yahangaika na joto kali

**LONDON,** Uingereza

WIMBI la joto kali linazidi kuitesa Ulaya Magharibi na kusababisha vifo vya watu na sehemu kubwa ya bara hilo kunyauka kutokana na jua kali.

Nchini Uingereza watabiri walisema rekodi ya kitaifa ya nyuzi 38.7 katika kipimo cha Celcius huenda ikavunjwa na kiwango cha nyuzi 40 ambacho kitarekodiwa kwa mara ya kwanza.

Wataalamu wanalaumu mabadiliko ya tabia nchi na kubashiri hali mbaya zaidi ya hali ya hewa. Wazima moto kusini magharibi mwa Ufaransa bado wanahangaika chini ya joto kali kujaribu kuzima moto katika maeneo mawili ambao ulisababisha uharibifu mkubwa.

Ireland imeshuhudia kiwango cha joto kikifikia nyuzi 33 Celcius, kiwango ambacho ni cha juu kabisa tangu mwaka 1887. Ubelgiji inatarajia kiwango cha joto cha kipindukia nyuzi 40. **DW**

## Punguzo bei unga laleta utata Kenya

**NAIROBI,** Kenya

SERIKALI ya Kenya kupitia Wizara ya Kilimo, imepunguza bei ya unga wa mahindi wiki nne kutoka shilingi 230 hadi shilingi 100.

Tangazo hilo lilieleza kuwa punguzo hilo la bei litaanza siku 20 kabla ya uchaguzi mkuu na kusababisha kuwapo na maswali kwa wananchi.

Watu wengi hasa mitandaoni wamehoji nia ya serikali kupunguza bei ya unga, ikizingatiwa kwamba kupanda kwa gharama ya unga imekuwa ikilalamikiwa kwa siku kadhaa.

Punguzo hilo ambalo sawa na asilimia 60, litadumu kwa wiki nne.

Mpango huo haujawekwa wazi na duru zinaarifu kuwa haujakamilishwa lakini utafanikishwa.

Tathmini katika sehemu nyingi za kuuza bidhaa hiyo inaonyesha bei haijapunguzwa .

Mpango huo wa ruzuku ya mahindi katika kipindi cha kampeni umechukuliwa na baadhi kama hatua ya Rais Uhuru Kenyatta, ambaye anamuunga mkono Raila Odinga kutoka Azimio la Umoja ili kuwashawishi wapiga kura.

Serikali pia imeondoa tozo zote zinazotozwa kwa mahindi kutoka nje ya nchi.

Wasindikaji watawauzia wafanyabiashara pakiti 12 za unga wa mahindi wa kilo 2 kwa Sh1,080, ambayo ina maana ya shilingi 90 kwa pakiti. Serikali itawafidia Sh1,120 kwa pakiti 12 za unga.

Naibu Rais William Ruto amemshutumu Rais Kenyatta kwa kucheza siasa na unga wa mahindi baada ya serikali kuchukua hatua zitakazopunguza bei ya bidhaa hiyo.

Akihutubia mikutano ya kampeni katika barabara jijini Nairobi, ambayo ina wapiga kura milioni 2.4.

Dk. Ruto alisema mkuu wa nchi aliingilia tu kuchukua hatua hiyo kama chombo cha kampeni kwa sababu uchaguzi umekaribia.

"Hii ni serikali ile ile ambayo hapo awali ililaumu bei ya juu ya bidhaa kwa vita vya Ukraine na Russia. Vita bado vinaendelea, kwa nini uliwaacha Wakenya wateseke kwa muda mrefu hivyo?" Ruto alihoji.

Aliongeza "Nimesikia wakisema watapunguza gharama ya unga. Mwenyekiti wa Azimio ndiye Rais na Raila ndiye anayepeperusha bendera. Ni tofauti gani unaweza kutarajia kutoka kwake? Serikali inataka kupunguza bei ya unga kwa sababu uchaguzi umekaribia." **BBC**

# AZAM YAFUNGA USAJILI NA BEKI MSENEGAL

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE klabu ya Azam FC imetangaza kufunga usajili wake baada ya kumtambulisha beki wa kati raia wa Senegal, Malickou Ndoye kutoka Teungueth FC ya nchini humo kwa mkataba wa miaka miwili.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Thabit Zacharia maarufu kama 'Zaka Zakazi' amesema jana kuwa mchezaji huyo anakuwa wa mwisho, huku wakitarajiwa kuungana naye kwenye kambi ya maandalizi ya msimu nchini Misri, akitokea Marekani.

**Ikumbukwe kuwa Teungueth ni klabu aliyotoka kiungo mshambuliaji wa Simba, Pape Sakho ambayo ilimsajili msimu uliopita.**

"Tayari tumeanza mazoezi na asilimia 98 ya wachezaji wameshafika, leo tumemtambulisha beki wetu mwingine na huyu ndiye atafunga usajili kwa ajili na msimu ujao. Ataungana na sisi nchini Misri akitokea Marekani, hata kipa wetu Ali Ahamada naye pia ataungana na sisi huko, ila kuna baadhi ya wachezaji ambao wanatajwa kufika hapa nchini kuanzia leo (jana), na tutaenda nao kambini huko Misri, hao ni Rodrers Kola, Prince Dube pamoja na Bruce Kangwa," alisema Zaka Zakazi.

Mchezaji huyo anakuwa wa tisa kusajiliwa kwa ajili ya msimu ujao, ambapo sita ni wageni na watatu wakiwa wazawa.

Mbali na Ndoye, wengine Kipre Junior na Tape Edinho raia wa Ivory Coaat, Issa Ndala kutoka Nigeria, James Akaminko ambaye ni Mghana, na Ali Ahmada kutoka nchini Comoro.

Wachezaji wa Kitanzania waliosajiliwa ni Nathaniel Chilambo kutoka Ruvu Shooting, Cleophace Mkandala kutoka Dodoma Jiji na Abdul Selemani 'Sopu' akisajiliwa kutoka Coastal Union.



Wacheza shoo wa bendi ya Mjomba, wakitoa burudani katika maonyesho ya 17 ya Vyuo Vikuu vya Tanzania (TCU), katika viwanja vya Mnazi Mmoja, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ruvu Shooting kuweka kambi Z'bar

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Simba ikiwa nchini Misri, Azam nayo ikitaraji kuelekea nchini humo na Yanga ikitangaza kubaki Kigamboni, Dar es Salaam, klabu ya Ruvu Shooting imetangaza kuweka kambi yake ya kujiandaa na msimu mpya wa ligi 'pre season' mjini Zanzibar.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Masau Bwire amesema wameamua kwenda Tanzania Visiwani kuweka kambi yao ili kuwaweka kwenye utulivu wachezaji wao, wajikite kwenye mafunzo ya mwalimu kupata nguvu na maarifa mapya kabla ya msimu ujao wa mashindano.

Masau alisema kwa sasa wapo kwenye usajili kabambe na ukifika muda watawatangazia mashabiki wa timu hiyo wachezaji waliowasajili na wale ambao wamewaacha.

"Tuko kwenye usajili wa bila makelele. Tunaelekea kwenye hatua za mwisho za kusajili, kuna siku maalum ambayo tutatangaza na wale tuliowaacha, na tumepanga kwenda Zanzibar, tumeamua tukajikite huko vijana wapambanane kujiandaa, wawe na nguvu mpya, maarifa mapya." Alisema Masau.

Alisema kuwa wanataka kutengeneza kikosi imara ambacho hawatopata tena presha kama waliokuwa nayo msimu uliopita.

"Sijawahi kupata tabu au presha kama nilivyopata msimu uliopita, ilibidi tuongeze nguvu za ziada ambayo ni maombi ili tusishuke daraja. Hadi tunawenda kucheza mechi za mwisho ilibidi tushinde zote, tunakwenda Songea kucheza na Mbeya Kwanza ambayo nayo inazihitaji pointi ili nayo isalie Ligi Kuu, haikuwa rahisi, ilinilazimu nifunge siku saba. Tulimuombea Mtibwa Sugar nayo ifungwe mechi zake mbili za mwisho ili tusiende kucheza mechi za mchujo 'play off', na kweli maombi yetu yalipokelewa kwa sababu walifungwa mabao 4-2 dhidi ya Namungo, halafu wakafungwa bao 1-0 dhidi ya Yanga, tukapona wakaenda wao kwenye 'play off', hili hatutaki lijirudie tena," alisema.

## Polisi kuanza mazoezi leo

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU Polisi Tanzania imesema leo inatarajia kuanza mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaoanza kutimua vumbi Agosti 17 mwaka huu.

Akizungumza jijini jana, Kocha msaidizi wa timu hiyo, George Mketo ambaye kipindi hiki atakuwa na timu mpaka hapo Kocha mkuu atakapopatikana, alisema wameamua kuanza kambi mapema kwa lengo la kuwaweka sawa wachezaji.

"Wachezaji wapo kambini kesho (leo) asubuhi tutaanza rasmi mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na msimu ujao," alisema Mketo.

Alisema baada ya kukaa kikao chao jana jioni watatoa tathmini yote kuelekea msimu huo, ikiwemo usajili pamoja na kutafuta michezo mbalimbali ya kirafiki.

"Leo jioni (jana) uongozi utakutana na kujadili mambo mbalimbali kuelekea msimu ujao hivyo baada ya kikao hicho nitawafahamisha kila kinachoendelea kwenye timu yetu," alisema.

Alisema kuhusu usajili wamewaongezea mikataba baadhi ya nyota wao wa zamani ambao bado wanawahitaji na kudai kwa wale ambao wamewasajili na waliowaacha watawatangaza hivi karibuni.

Timu hiyo imeweka kambi yake Kurasini, Dar es Salaam.

## Timu ya soka la ufukweni kupaa Malawi

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Taifa ya Soka la ufukweni (Beach Soccer) kesho inatarajiwa kuelekea nchini Malawi kwa ajili ya mchezo wao wa kuwania kufuzu michuano ya mataifa ya Afrika utakaopigwa Jumamosi.

Akizungumza jijini jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Boniface Pawasa alisema maandalizi kuelekea kwenye mchezo huo yanaendelea vizuri na wameamua kuondoka mapema kutokana na changamoto ya usafiri.

"Tunaendelea vizuri na mazoezi kwa ajili ya mchezo wetu dhidi ya Malawi, kwani naamini mchezo utakuwa mgumu na wa ushindani, lakini tumejipanga vizuri," alisema Pawasa.

Alisema wachezaji wake wanaendelea vizuri na hadi sasa hana mchezaji yeyote ambaye amepata majeraha.

Alisema anaendelea kuwapa wachezaji wake mazoezi ya pumzi ili waendelee kuwa sawa kuelekea kwenye mchezo wao huo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RONALDO ANUKIA ATLETICO

KLABU ya Atletico Madrid imewasiliana na wawakilishi wa Cristiano Ronaldo kuhusu kumsajili mshambuliaji huyo wa Ureno, 37, kutoka Manchester United. ***(AS)***

### RONALDO KUONGEZA MWAKA

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag anadai Cristiano Ronaldo anaweza kusalia Old Trafford zaidi ya mwaka ambao amebakisha kwenye mkataba wake. ***(Guardian)***

### KOUNDE SAFI CHELSEA

KLABU ya Chelsea tayari imefikia makubaliano kibinafsi na Jules Kounde na sasa wametoa euro milioni 55 kwa Sevilla kumnunua beki huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 23. ***(Marca)***

### RAMSEY KUONDOKA

KIUNGO wa kati wa Wales, Aaron Ramsey mwenye umri wa miaka 31, yuko kwenye mazungumzo na Juventus ili kumaliza mwaka wa mwisho wa mkataba wake na kumruhusu kusaini na klabu nyingine bila malipo. ***(Mail)***

### DE LIGT RASMI BAYERN

MLINZI wa Uholanzi, Matthijs de Ligt mwenye umri wa miaka 22 amewasili Ujerumani kukamilisha uhamisho wake kutoka Juventus kwenda Bayern Munich baada ya klabu hizo kukubaliana ada ya euro milioni 70 pamoja na euro milioni 10 za nyongeza. ***(Corriere dello Sport)***

### ONANA AWINDWA

KLABU ya West Ham ina uhakika wa kumsajili kiungo wa kati wa Lille na Ubelgiji, Amadou Onana mwenye umri wa miaka 20, baada ya kutuma ofa mpya ya takriban pauni milioni 30 pamoja na nyongeza. Wagonga nyundo hao pia wanavutiwa na mchezaji wa zamani wa mkopo, Jesse Lingard, huku mshambuliaji huyo wa England mwenye umri wa miaka 29, sasa yupo huru baada ya kuondoka Manchester United. ***(Standard)***

### D JONG MAMBO BADO

BARCELONA bado wanakataa kujitolea kumlipa kiungo wa kati wa Uholanzi, Frenkie de Jong, 25, euro milioni 17 katika mkataba wake uliorekebishwa, na kuendeleza mzozo juu ya uwezekano wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 kwenda Manchester United. ***(Independent)***

### TERRIER AGOMBEWA

LEEDS United na West Ham zina nia ya kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Martin Terrier, 25, kutoka Rennes, ambaye wanataka angalau euro milioni 40 kwa mchezaji huyo. ***(L'Equipe)***


### SILVA KUTUA ANDERLECHT

MSHAMBULIAJI wa Wolves, Fabio Silva, 19, yuko mbioni kufanyiwa vipimo vya afya na Anderlecht baada ya kukubali kujiunga na Ubelgiji kwa mkopo. ***(Fabrizio Romano)***

### PAQUETA ANUKIA ARSENAL

MATUMAINI ya Arsenal kumsajili kiungo wa kati wa Brazil, Lucas Paqueta, 24, yametiwa nguvu huku Lyon ikiwa imeshuka bei yake. ***(Media Foot)***

## DONDOO ... OKA
## MAGAZET ... AYA



# INTER MIAMI SASA KUMSAJILI MESSI

## ●●● Lengo ni kuimarisha soka la Marekani, huku Beckham akipambana kuhakikisha...

**NEW YORK,** Marekani

LIONEL Messi akihamia klabu ya Ligi Kuu ya soka ya Marekani, MLS, Inter Miami itatumika kama "kuimarika kwa soka la Marekani," wakati mmiliki mwenza wa klabu hiyo, David Beckham akitaka kusajili wachezaji wenye majina makubwa duniani.

**Huo ni ujumbe kutoka kwa ofisa mkuu wa biashara wa Miami, Xavier Asensi, ambaye alidokeza kwa gazeti la Mundo Deportivo kwamba, timu yake inapanga kumsajili Messi.**

Gareth Bale na Giorgio Chiellini walichezea mechi yao ya kwanza kwa Los Angeles FC ya MLS Jumapili katika ushindi wa 2-1 dhidi ya Nashville SC.

Mshindi mara tano wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Bale na Chiellini aliyeshinda taji la Euro 2020 akiwa na Italia mwaka jana, walijiunga na Wayne Rooney, Zlatan Ibrahimovic na Beckham kama baadhi ya wachezaji wenye majina makubwa kucheza MLS.

Huku mkataba wa Messi na Paris Saint-Germain ukitarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu ujao, Asensi amependekeza Miami kujaribu kumsajili Messi.

Alipoulizwa kama kusajili mchezaji kama Messi kunalengwa na Beckham, Asensi alisema: "Ndiyo, kwa tahadhari. Huwezi kumlinganisha Leo Messi na mchezaji mwingine yeyote; yeye ni tofauti.

"Baada ya kusema hivyo, tunachotafuta ni kuwa sehemu ya kumbukumbu ya mpira wa miguu hapa Marekani na kufanya hivyo, jambo muhimu ni wachezaji wakubwa.

"Ili kufanya hivyo, unahitaji wachezaji bora, na kuwa nao ni lengo la kweli katika klabu hii.

"Inategemea yeye na kile anachotaka. Tunataka kuwa na wachezaji bora zaidi duniani, na nadhani Messi ndiye bora zaidi katika historia."

Messi mwenye umri wa miaka 35, alikuwa na msimu wa kwanza mgumu katika viunga vya PSG, akifunga mabao 11 katika mechi 34 katika mashindano yote.

BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,016,4

JACKPOT

MECHI WIKI HII

TAREHE: 20-21 JULAI 2022

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 20/07/22 | 18:00 | CA Fenix vs Mvo Wanderers | 2.39 | 3.02 | 3.12 |
| 02. 20/07/22 | 20:00 | Maccabi Haifa vs Olympiakos | 3.16 | 3.11 | 2.37 |
| 03. 20/07/22 | 20:00 | San Lorenzo vs Union Santa Fe | 2.44 | 3.18 | 3.07 |
| 04. 20/07/22 | 20:00 | Botev Plovdiv vs Apoel Nicosia | 2.88 | 3.23 | 2.42 |
| 05. 20/07/22 | 21:00 | Dynamo Kiev vs Fenerbahce | 2.75 | 3.30 | 2.55 |
| 06. 20/07/22 | 21:15 | Maribor vs Sheriff Tiraspol | 2.79 | 3.09 | 2.64 |
| 07. 21/07/22 | 01:00 | Goias vs Fluminense | 3.24 | 3.19 | 2.26 |
| 08. 21/07/22 | 01:00 | CSA AL vs Cruzeiro | 3.18 | 2.93 | 2.41 |
| 09. 21/07/22 | 01:00 | Defensa Justicia vs Independiente | 2.30 | 3.23 | 3.28 |
| 10. 21/07/22 | 02:30 | Internacional vs Sao Paulo | 2.34 | 3.14 | 3.14 |
| 11. 21/07/22 | 03:30 | Lanus vs Velez Sarsfield | 2.82 | 3.12 | 2.67 |
| 12. 21/07/22 | 05:05 | Guadalajara Chivas vs Club Leon | 2.26 | 3.24 | 3.19 |
| 13. 21/07/22 | 20:30 | Aris Limassol vs Neftchi Baku | 2.37 | 3.16 | 3.01 |

KUWEKA PESA:

- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa | vodacom m-pesa | halopesa | airtel money | ZANTEL EZYPESA

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

18+

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# MAGUIRE AONYWA KUHUSU KIWANGO

**MANCHESTER,** England

KOCHA Erik ten Hag amemwonya Harry Maguire kwamba, ni lazima athibitishe kuwa yeye ni bora na anastahili kucheza mara kwa mara katika safu ya ulinzi ya Manchester United.

Maguire alivumilia kampeni ngumu ndani na nje ya uwanja msimu uliopita, na kusababisha mapendekezo ya David de Gea au Cristiano Ronaldo angechukua nafasi ya unahodha wa United.

Hata hivyo, Ten Hag alifafanua katika mkutano na waandishi wa habari wakati wa ziara ya United ya kujiandaa na msimu mpya nchini Thailand na Australia kwamba, mchezaji huyo wa kimataifa wa England ataendelea kuvaa kitambaa hicho.

Hiyo ilionekana kuwa kura kubwa ya imani kwa Maguire, ingawa sasa anakabiliwa na ushindani wa ziada wa nafasi ya kuanza baada ya ujio wa Lisandro Martinez kutoka Ajax.

United wamefikia makubaliano ya pauni milioni 56.5 na mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Uholanzi, Eredivisie, kumnunua Martinez, ambaye anaweza kucheza nafasi kadhaa lakini anapenda zaidi kucheza beki wa kati.

Hiyo ingemfanya kucheza pamoja na Raphael Varane, huku Victor Lindelof pia akipigania nafasi hiyo.

Ingawa Ten Hag amesisitiza kuwa yeye ni shabiki wa Maguire, Mholanzi huyo hajampa nahodha wake uhakikisho wowote kuelekea msimu mpya.



## Afurahia kuungana na Koulibaly

**LONDON,** England

KIUNGO wa kati wa Chelsea Jorginho amemsifu mchezaji mpya aliyesajiliwa Kalidou Koulibaly kama "kiongozi halisi" huku akielezea kufurahishwa kwake na kuunganishwa tena na mchezaji mwenzake wa zamani wa Napoli hapo Stamford Bridge.

Klabu hiyo ya Ligi Kuu ya England ilimsajili Koulibaly wiki iliyopita kwa ada iliyoripotiwa kuwa ya pauni milioni 33.8, huku nahodha huyo wa Senegal akisaini mkataba wa miaka minne.


Koulibaly alicheza mechi 236 za Serie A katika kipindi cha miaka minane akiwa na Napoli, na kuwasaidia kumaliza katika nafasi ya pili na kutwaa ubingwa wa Coppa Italia mara moja.

Jorginho alicheza pamoja na Koulibaly katika misimu minne ya kwanza ya beki huyo nchini Italia, na wawili hao sasa wanatarajiwa kuungana England.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia amefichua kuwa alizungumza kuhusu kuungana tena na Koulibaly mara kadhaa baada ya kuhamia London mwaka 2018, huku akimsifu beki huyo kwa uwezo wake wa uongozi.

## HABARI MICHEZO


28,582/-

# YASSIN WA YANGA SC ATUA SINGIDA BIG STARS

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Singida Big Stars bado haishikiki kwenye usajili na sasa imemsajili beki wa kushoto, Yassin Mustapha ambaye ameachwa na Yanga.

**"Tumefanikiwa kunasa beki wa kushoto mahiri kutoka Yanga kwa mkataba wa miaka miwili," klabu hiyo iliandika kwenye mtandao wake wa instagram.**

Huyo anakuwa mchezaji wa tano kwa timu hiyo ambayo ilipanda daraja msimu huu kwa kutumia jina la DTB, kabla ya kubadilisha.

Wachezaji wengine ambao wamesajiliwa na klabu hiyo ni Metacha Mnata kutoka Polisi Tanzania, Abdulmajid Mangalo kutoka Biashara United, Kelvin Sabato kutoka Mtibwa Sugar na Aziz Andambwile kutoka Mbeya City.

Wakati huo huo, klabu ya Dodoma Jiji imeedelea kufanya usajili wa 'kufa mtu', safari hii ikiwanyakua straika Hassan Mwaterema kutoka Kagera Sugar na golikipa Daniel Mgore kutoka Biashara United.

Hao ni wachezaji tisa kusajiliwa, kati ya 10 wapya ambao Katibu Mtendaji wa klabu hiyo Furtunatus John aliahidi kuwasajili msimu huu.

Mbali na wachezaji hao, Dodoma Jiji imewasainisha Jimmy Shoji kutoka Mbeya Kwanza na Rashid Chambo kutoka Coastal Union.

Huo ni mfululizo wa klabu hiyo kuendelea kujiimarisha, kwani tayari ilikuwa imewasajili Amani Kyata kutoka Coastal Union, Paul Peter kutoka Azam FC, Randy Bangala kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Collins Opare na Christian Ziggah kutoka Biashara United.



Wachezaji wa Simba wakiwa kwenye mazoezi ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa mjini Ismailia nchini Misri, jana. **PICHA: SIMBA**

# *Vipaji vingi kuibuka netiboli Klabu Bingwa*

**Na Shufaa Lyimo**

MJUMBE wa Kamati ya Utendaji ya Chama cha Mchezo wa Netiboli Tanzania (CHANETA) ambaye ni Mwenyekiti wa timu ya Taifa ya mchezo huo, Ray Kilongozi amesema kupitia mashindano ya Klabu Bingwa Ligi Daraja la Kwanza watafanikiwa kupata timu ya Taifa ambayo itakwenda kushiriki mashindano nchini Afrika Kusini.

Akizungumza jijini jana, Kilongozi alisema tangu mashindano hayo yaanze ameona vipaji vingi hususani kwa upande wa wachezaji chipukizi.

"Tangu mashindano haya yaanze nimeona vipaji vingi hasa kwa wachezaji chipukizi, nina amini tutakuwa na timu bora ya Taifa," alisema Kilongozi.

Alisema awali walitarajia timu zaidi ya 20 zishiriki lakini zimeshindwa kutokana na ukata wa fedha, hivyo kuzitaka zijipange upya kwa ajili ya msimu ujao.

"Kwa upande wa timu ambayo hazijaweza kushiriki mashindano haya zijipange kwa ajili ya mashindano ya msimu ujao," alisema mwenyekiti huyo.

Alisema kwenye mashindano hayo zitapatikana timu ambazo zitashiriki mashindano ya Muungano, na baadhi ya wachezaji wataitwa kwenye timu ya Taifa.


SUPA JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23/07/22 | 19:15 | Kortrijk vs OH Leuven | 2.39 | 3.48 | 2.79 |
| 02. 23/07/22 | 21:30 | Hannover vs St. Pauli | 2.38 | 3.43 | 2.83 |
| 03. 23/07/22 | 21:30 | Sarmiento vs Colon Santa Fe | 2.42 | 3.14 | 3.14 |
| 04. 23/07/22 | 22:30 | Vila Nova GO vs Vasco da Gama | 2.63 | 2.73 | 3.08 |
| 05. 24/07/22 | 00:30 | Nautico PE vs Londrina PR | 2.30 | 2.97 | 3.36 |
| 06. 24/07/22 | 02:30 | CRB AL vs Novorizontino SP | 2.48 | 2.93 | 3.08 |
| 07. 24/07/22 | 02:30 | FC Cincinnati vs Nashville | 2.32 | 3.42 | 3.02 |
| 08. 24/07/22 | 02:30 | Orlando City vs Philadelphia Union | 2.37 | 3.43 | 2.93 |
| 09. 24/07/22 | 03:00 | Botafogo RJ vs Atletico Pr | 2.30 | 3.33 | 3.03 |
| 10. 24/07/22 | 03:00 | DC United vs Montreal Impact | 2.31 | 3.38 | 3.07 |
| 11. 24/07/22 | 03:30 | Sporting Kansas City vs Los Angeles FC | 2.90 | 3.50 | 2.35 |
| 12. 24/07/22 | 05:00 | Vancouver Whitecaps vs Chicago Fire | 2.28 | 3.45 | 3.05 |
| 13. 24/07/22 | 12:00 | Tokyo Verdy vs Yokohama | 2.90 | 3.30 | 2.42 |
| 14. 24/07/22 | 14:30 | Karlsruher SC vs Magdeburg | 2.50 | 3.40 | 2.70 |
| 15. 24/07/22 | 17:00 | Mechelen vs Royal Antwerp | 2.55 | 3.40 | 2.65 |
| 16. 24/07/22 | 22:00 | Westerlo vs Cercle Brugge | 2.68 | 3.28 | 2.58 |
| 17. 24/07/22 | 22:00 | Juventude RS vs Ceara CE | 2.58 | 2.98 | 2.93 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 20/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2610 | Hoang Anh Gia Lai vs B. Binh Duong | 1.64 | 3.65 | 5.20 |
| 13:00 | 2983 | Tokyo Verdy vs Jubilo Iwata | 2.55 | 3.18 | 2.55 |
| 13:00 | 3907 | Uttar Baridhara Club vs Abahani Ltd. Chittagong | 4.02 | 3.73 | 1.72 |
| 13:00 | 4172 | China vs South Korea | 12.69 | 9.37 | 1.09 |
| 13:00 | 5883 | Lambton Jaffas vs Lake Macquarie City FC | 1.09 | 8.44 | 15.70 |
| 15:15 | 1155 | TT Ha Noi vs SAI Gon FC | 1.53 | 3.79 | 5.52 |
| 15:15 | 3413 | Ho Chi Minh City vs Hong Linh HA Tinh FC | 2.20 | 3.20 | 3.00 |
| 16:00 | 2808 | Gimnasia de la Plata Reserve vs CA River Plate (Arg) | 2.76 | 3.25 | 2.33 |
| 16:00 | 4020 | Velez Sarsfield Reserve vs CA Lanus | 2.17 | 3.15 | 3.10 |
| 16:00 | 4464 | Penang vs Johor Darul Takzim | 8.99 | 5.47 | 1.24 |
| 16:00 | 5303 | Melaka vs FC Petaling Jaya City | 1.58 | 3.78 | 4.91 |
| 16:00 | 5833 | Selangor FC vs Kuala Lumpur | 1.90 | 3.64 | 3.35 |
| 17:00 | 3949 | CA Barracas Central Reserve vs Estudiantes de LP Reserve | 3.35 | 3.25 | 2.03 |
| 17:00 | 4696 | CA Aldosivi Reserve vs Colon de Santa Fe Reserve | 2.60 | 3.09 | 2.55 |
| 17:00 | 5045 | Chivas Guadalajara U20 vs Leon U20 | 2.19 | 3.13 | 3.08 |
| 18:00 | 5652 | CA Fenix vs Mvo Wanderers | 2.37 | 3.00 | 2.90 |
| 18:30 | 3100 | FF Jaro vs Kerho 07 | 1.50 | 4.23 | 5.12 |
| 19:00 | 3008 | FC Vaajakoski vs GBK Kokkola | 1.69 | 4.21 | 3.67 |
| 19:00 | 5065 | HJK Helsinki vs Viktoria Plzen | 3.75 | 3.35 | 1.94 |
| 20:00 | 1012 | Maccabi Haifa vs Olympiakos | 2.85 | 3.10 | 2.47 |
| 20:00 | 1025 | Crucero Del Norte vs Racing De Cordoba | 5.10 | 3.09 | 1.72 |
| 20:00 | 1114 | Gottne IF vs Friska Viljor FC | 2.50 | 3.75 | 2.41 |
| 20:00 | 1185 | Def Pronunciamiento vs Central Norte Salta | 3.88 | 2.90 | 2.01 |
| 20:00 | 1914 | Botev Plovdiv vs Apoel Nicosia | 3.34 | 3.24 | 2.17 |
| 20:00 | 1970 | Ferro Carril Oeste GP vs Estudiantes SL | 2.14 | 2.80 | 3.63 |
| 20:00 | 2478 | San Lorenzo vs Union Santa Fe | 2.34 | 2.90 | 3.05 |
| 20:30 | 3689 | SV Erlbach vs TSV 1860 II | 2.79 | 3.57 | 2.16 |
| 21:00 | 1079 | Union Sunchales vs Def Belgrano VR | 2.39 | 2.69 | 3.22 |
| 21:00 | 1411 | Dynamo Kiev vs Fenerbahce | 2.85 | 3.20 | 2.40 |
| 21:00 | 1827 | Ciudad de Bolivar vs Villa Mitre | 2.70 | 2.65 | 2.84 |
| 21:00 | 1971 | Sportivo Penarol vs Atletico Camioneros | 2.29 | 2.60 | 3.58 |
| 21:00 | 2025 | Circulo Deportivo vs Sol de Mayo | 2.79 | 2.70 | 2.70 |
| 21:00 | 2034 | Huracan Las Heras vs Desamparados | 2.25 | 2.75 | 3.43 |
| 21:00 | 2651 | Sansinena vs Cipolletti | 2.07 | 2.70 | 4.03 |
| 21:00 | 3009 | Vikingur Gota vs Dunajska Streda | 3.48 | 3.43 | 2.04 |
| 21:00 | 3802 | Boca Unidos vs Juventud Unida G | 1.81 | 3.25 | 4.14 |
| 21:00 | 3879 | Juventud Unida SL vs Club Olimpo | 3.20 | 2.51 | 2.56 |
| 21:00 | 4178 | Ferencvaros TC vs Slovan Bratislava | 1.40 | 4.39 | 7.38 |
| 21:15 | 4559 | Maribor vs Sheriff Tiraspol | 2.67 | 2.97 | 2.72 |
| 21:45 | 1023 | Hibernian vs Morton | 1.15 | 5.91 | 15.77 |
| 21:45 | 2574 | Edinburgh City vs Cowdenbeath | 1.26 | 5.30 | 8.64 |
| 21:45 | 5690 | Bonnyrigg Rose vs Falkirk FC | 2.52 | 3.40 | 2.45 |
| 22:00 | 1049 | Sutjeska vs KI Klaksvik | 2.47 | 3.22 | 2.82 |
| 22:00 | 4041 | CA Boston River vs Cerro Largo FC | 2.07 | 3.10 | 3.39 |
| 22:00 | 4493 | Wydad Casablanca vs FUS Rabat | 2.21 | 3.04 | 3.14 |
| 22:00 | 4494 | England W vs Spain W | 1.92 | 3.39 | 3.54 |
| 22:30 | 3068 | Patronato Parana vs CA Tigre | 2.66 | 3.00 | 2.56 |
| 23:00 | 2379 | Firpo vs Once Municipal | 2.04 | 2.99 | 3.63 |
| 23:00 | 2561 | Chacaritas FC vs Manta | 1.74 | 3.29 | 4.52 |
| 23:30 | 4127 | Liga Deportiva Alajuelense vs Santos Guapiles | 1.54 | 4.10 | 5.40 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatano Julai 20, 2022

Nipashe




Inter Miami kumsajili Messi

UKURASA 21



Mchezaji wa Timu ya Taifa Stars, Dickson Kibabage (kulia), akiwania mpira dhidi ya wachezaji wa Sudan Kusini, wakati wa mchezo wa kirafiki baina ya timu hizo wa kujiandaa na mashindano ya mataifa ya Afrika kwa wachezaji wa ndani (CHAN) katika Viwanja vya Jakaya Kikwete, Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Poulsen na mikakati Stars kufuzu CHAN

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Taifa Stars, Kim Poulsen, amesisitiza kufanya vikao vya mara kwa mara na wachezaji wake kambini kwa ajili ya kupanga mipango mikakati ya kushinda michezo miwili dhidi ya Somalia ya kufuzu michuano ya Mataifa ya Afrika kwa wachezaji wa ndani (CHAN).

Stars iko kambini kujiandaa na michezo hiyo huku wakianzia nyumbani kwa kucheza Julai 23, mwaka huu (Jumamosi hii), Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam na Julai 30, watacheza mchezo wa marudiano.

Akizungumza na gazeti hili jana, Poulsen alisema mikakati yake ni kuhakikisha wanafanya vizuri na hatimaye kufuzu kwa michuano hiyo kwa mwakani ambayo yanayotarajiwa kufanyika Algeria.

Alisema hawawezi kufika huko hadi pale watakapofanya vizuri katika michezo hiyo miwili na baadaye kwenda kutafuta matokeo mazuri katika mchezo wa hatua ya pili dhidi ya Uganda.

"Tumekuwa na vikao vya mara kwa mara na wachezaji wangu kuhusu mipango mikakati yetu katika michezo hii miwili kuhakikisha tunashinda mechi zote mbili dhidi ya Somalia na baadaye dhidi ya Uganda.

"Tunahitaji kufuzu kufikia huko lazima wachezaji wapambaane na kushinda mechi zote zilizoko mbele yetu nina imani na wachezaji kwa sababu kila mmoja anatambua muhimu wa kutafuta ushindani katika hizi mechi," alisema Poulsen.

Alisema wanaendelea vizuri na maandalizi na wanaendelea kupata mechi za kirafiki kwa ajili ya kuwa nafasi kila mchezaji kuwa na utayari kwa ajili kupata mwanga wa kikosi chake na utayari kwa wachezaji wake.

# Chico, Yacouba watemwa Yanga

**Na Saada Akida**

## ●●● Leo kuanza kambi yake Kigamboni, Siku ya Wananchi Agosti Mosi, kilele Agosti 6...

KLABU ya Yanga imefikia makubaliano ya kuachana na nyota wake wawili wa kigeni, Chico Ushindi, Yacouba Songne na hawatakuwa sehemu ya kikosi cha timu hiyo kwa msimu wa 2022/23.

**Kutemwa kwa wachezaji hao kunaifanya Yanga kubakiwa na wachezaji 12 wa kigeni kama kanuni za Shirikisho la Soka Tanzania, TFF, inavyosema ambapo awali walikuwa 14 baada ya kuongeza wachezaji watano katika usajili wao wa sasa.**

Kuondoka kwa mastaa hao, kunafanya wachezaji wa kigeni waliobaki kuwa ni Djigui Diarra, Djuma Shaban, Yanick Bangala, Khalid Aucho, Jesus Moloko, Fiston Mayele, Heritier Makambo, Stephane Aziz Ki, Bernard Morrison, Gael Bigirimana, Joyce Lomalisa na Lazarous Kambole.

Kwa upande wa wachezaji wa ndani, ambao tayari wameshapewa mkono wa kwaheri ni Balama Mapinduzi, Deus Kaseke, Yassin Mustafa na Paul Godfrey.

Akizungumza na gazeti hili jana, Msemaji wa Yanga, Haji Manara alisema Chico alikutana na wakafikia makubaliano ya yeye kurejea katika klabu yake ya awali ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).

Alisema nyota huyo amerejea katika klabu yake ya zamani na Songne ameitwa mezani ili kumalizana nae, na hii ni kutokana kuwa majeruhi kwa muda mrefu hali inayomfanya asiweze kuwa fiti kwa asilimia 100 kwa mujibu wa daktari.

"Songne hajawa fiti kwa asilimia 100, ila tumemuita kwa ajili ya kufikia makubaliano kwa sababu daktari ametushauri anatakiwa kuendelea kupata programu maalum ili kuwa fiti zaidi na kurejea katika ubora wake," alisema Manara.

Alisema nyota hao hawatakuwa sehemu ya kikosi kitachoingia kambini leo na kwa muda wote wachezaji walipewa programu maalum kabla ya kurejea kambini.

"Tumechelewa kambini kwa sababu ya kufuata maelekezo ya benchi la ufundi kwa kuhitaji wachezaji kupata muda wa kutosha wa kupumzika kwa sababu msimu uliopita hawakupata nafasi hiyo.

"Kwa muda wote Kocha Nasreddine Nabi alitoa programu maalum kwa wachezaji wote kipindi wako nyumbani kwa ajili ya kujiweka fiti na kuwa tayari kwa ajili ya 'pre-season' ambayo itakuwa jijini Dar es Salaam katika kambi yetu ya Avic Town," alisema Manara.

Alisema timu hiyo itafanya maandalizi yake ya msimu mpya hapa nchini na inategemea programu za kocha wao na kuhusu mechi za kirafiki itatangazwa baadaye.

"Ni kweli tulikuwa na mipango ya kwenda nchini Uturuki, lakini kutokana na muda kutokuwa rafiki tukalazimika kufuta safari hiyo kwa sababu ya ushauri wa benchi la ufundi na kuhusu taarifa za deni kwamba kuna kampuni inatudai fidia hizo hazijatufikia," alisema Manara.

Alisema wiki ijayo watazindua jezi mpya za msimu mpya, lakini Siku ya Wananchi itaanza rasmi Agosti Mosi na 6 itakuwa kilele chake.

"Siku hiyo tutacheza na mabingwa wenzetu ila wanatoka wapi ni siri yetu na tutakuja kutangaza hapo baadaye," alisema Manara.

Wakati Manara hakuweka wazi timu watakayocheza nao ila gazeti hili linataarifa kwamba, Yanga inatarajia kucheza na Red Arrows ya Zambia mchezo wa kirafiki wa kimataifa katika siku yao hiyo inayotarajiwa kufanyika Agosti 6.

Red Arrows ni mabingwa wa Zambia kwa msimu uliopita wa 2021/23 wakiwa na michezo 34, wakishinda 20, sare 10 na kupoteza minne.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >